**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# HOTUBA YA WAZIRI WA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## MHESHIMIWA: BALOZI ALI ABEID KARUME (MBM)

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**JUNI, 2020**

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........................................................................1
2.0MUHTASARI WA MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI
CHA MAPINDUZI MIAKA MITANO 2015-2020..................................3
3.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA
WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA
MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020................................................5
4.0 MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA
WA 2020/2021 ..........................................................................30
4.1 MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA
WA 2020/2021 ..........................................................................30
5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA
NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ..............................31
6.0 SHUKRANI ...............................................................................40
7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU
ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021........................41
VIAMBATANISHO .........................................................................42
KIAMBATISHO NAMBA 1 A
FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2019 HADI MACHI 2020
KWA MATUMIZI YA KAWAIDA .........................................................43
KIAMBATISHO NAMBA 1B
MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2019 HADI MACHI 2020
MAPATO YANAYOINGIA HAZINA.....................................................45
KIAMBATISHO NAMBA 1C
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA ...............................46
KIAMBATISHO NAMBA 1D
FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 KWA
KILA PROGRAMU NDOGO .............................................................46
KIAMBATISHO NAMBA 1E
FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 KWA

KILA PROGRAMU NDOGO ........................................................ 48
KIAMBATISHO NAMBA 1F
BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ........................... 49
KIAMBATISHO NAMBA 1G
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO ........................................................ 51
KIAMBATISHI NAMBA 1H
MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 MAPATO YANAYOINGIA HAZINA ................................................ 52
KIAMBATISHO NAMBA 1I
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA ................................ 52
KIAMBATISHO NAMBA 2
UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MIPINDUZI KWA KIPINDI CHA MIAKA 52015-2020 ........................................................ 53
KIAMBATANISHO NAMBA 3A
VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOFAIDIKA NA PEMBEJEO ZA KILIMO UNGUJA NA PEMBA ........................................................ 63
KIAMBATANISHO NAMBA 3B
VIKUNDI VYA VIJANA VITAKAVYOFAIDIKA NA VIFAA VYA USHONI UNGUJA NA PEMBA ................................................ 64
KIAMBATANISHO NAMBA 3C
MCHANGANUO WA VITALU NYUMBA PAMOJA NA VISIMA NA MIUNDOMBINU YA MAJI UNGUJA NA PEMBA .............................. 65
KIAMBATANISHO NAMBA 3D
VIKUNDI VYA WATU WENYE ULEMAVU VILIVYOFAIDIKA NA VIFAA UNGUJA NA PEMBA ................................................ 67
KIAMBATANISHO NAMBA 4 ................................................ 69

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, MHESHIMIWA BALOZI ALI ABEID KARUME (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima, afya njema, uwezo na nguvu za kutekeleza yale yote tuliojipangia katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Vile vile, kwa rehema zake Mwenyezi Mungu ametuwezesha kukutana hapa leo katika Baraza hili tukufu tukiwa salama katika hali ya amani na utulivu kwa ajili ya kuiwasilisha na kuijadili bajeti hii.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee na kwa dhati kabisa naomba kumpongeza **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein,** ambaye pia ni **Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)** kwa kufikisha miaka tisa ya uongozi wake, ambapo sote tunashuhudia maendeleo yaliyopatikana chini ya uongozi wake katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie afya na uzima ili aweze kukamilisha utekelezaji wa Sera ya Chama Cha Mapinduzi ya 2010-2020 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 kwa salama na amani.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, **Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi** kwa kumsaidia vyema **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** katika kuimarisha ufanisi na uwajibikaji katika shughuli za Serikali. Vile vile, naomba kumpongeza kwa kuongoza shughuli za Serikali kwa ufanisi mkubwa sana hasa kwenye shughuli za Baraza la Wawakilishi.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kukupongeza kwa dhati wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa kuongoza vyema mhimili huu Mkuu wa Serikali kwa kipindi chote cha miaka mitano (5) kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa. Vile vile, naomba kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, hasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ya kusimamia Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

6. **Mheshimiwa Spika,** kama tujuavyo Taifa letu limekumbwa na ungojwa wa COVID-19 ambao unasumbua dunia nzima kwa sasa. Tuendelee kuwaomba wananchi wote wa Zanzibar kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na Serikali kupitia Wizara zetu mbili za Afya za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania (SMT) katika kujilinda na maambukizi ya ugonjwa huo. Napenda pia kuwapongeza sana madaktari, wauguzi na wale wote waliopo mstari wa mbele katika mapambano haya. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuvushe salama katika mtihani huu wa maradhi unaoikabili dunia kwa sasa.

## 2.0 MUHTASARI WA MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO 2015-2020

7. **Mheshimiwa Spika,** kama tujuavyo bajeti ya mwaka huu ndio bajeti ya mwisho katika kipindi cha pili cha miaka mitano, chini ya Uongozi wa **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein.** Naomba kuchukua nafasi hii kuelezea kwa muhtasari baadhi ya mafanikio makubwa ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kipindi cha miaka mitano, kama ifuatavyo: -

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Vijana, Wizara imepata mafanikio kwa kuongeza idadi ya vijana katika Mabaraza ya Vijana ambapo idadi ya wanachama imefikia 17,540 wakiwemo wanawake 9,189 na wanaume 8,351 kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba ikilinganishwa na idadi ya 6,132 kwa mwaka 2015 ambapo wanawake 3,214 na wanaume 2,918. Kuanza kwa Programu ya Ajira kwa Vijana ambapo jumla ya vijana 3,300 Unguja 2,102 na Pemba 1,198 wameanza kunufaika na programu hiyo kwa awamu ya kwanza katika maeneo ya kilimo, ushonaji, mafunzo kazi na uendelezaji wa michezo.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuwajengea uwezo viongozi na wanachama wa Mabaraza ya Vijana wapatao 2,559. Aidha, vijana 23,895 kwa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya uzalendo, ujasiriamali, elimu ya stadi za maisha katika maeneo ya afya ya uzazi, UKIMWI, madawa ya kulevya na athari za mimba za utotoni.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Utamaduni na Sanaa, Kongamano la Kimataifa la lugha ya Kiswahili limekuwa likifanyika kwa mara ya tatu mfululizo kwa kushirikisha wataalamu na wasomi wa Kiswahili kutoka ndani na nje ya nchi wapatao 656. Makala za kitaalamu za Kiswahili ziliwasilishwa na kujadiliwa na baadae wataalamu hao walifikia maazimio ya kuimarisha lugha ya

Kiswahili ili kutoa fursa zaidi na kuchangamkia fursa zilizopo. Aidha, naomba kumpongeza **Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein,** kwa kukamilisha azma yake ya kuanzisha Studio ya Filamu na Muziki ya Rahaleo ambapo wasanii, Taasisi za Serikali na binafsi wamekuwa wakiitumia kwa shughuli mbalimbali za sanaa na kijamii.

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuadhimisha tamasha la utamaduni wa Mzanzibari, kila mwaka ambapo shughuli za kiutamaduni hufanyika sambamba na kuratibu matamasha ya utamaduni ya kijamii katika kukuza na kuendeleza utamaduni na utalii. Vile vile, kukiimarisha na kukiendeleza kikundi cha Taifa cha Taarab kwa kukipatia vifaa na ofisi ya kufanyia shughuli zao. Aidha, Wasanii wamepatiwa fursa mbalimbali za masomo pamoja na kupatiwa vifaa ili kuendeleza shughuli zao za sanaa. Katika kuhakikisha maslahi ya wasanii yanaimarika, jumla ya **shilingi 354,274,166/=** za mirabaha zimekusanywa kutoka kwa watumiaji mbalimbali na kugaiwa kwa wasanii na wabunifu 5,028 wa Unguja na Pemba.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Michezo, Wizara imefanikiwa kufanya matengenezo makubwa ya kiwanja cha michezo cha Mao - Zedung na kimeanza kutumika kwa mchezo wa mpira wa miguu, mpira wa meza (table tenis), mchezo wa kikapu (basketball) na sehemu ya kufanyia mazoezi ya viungo. Vile vile, Ujenzi wa viwanja vitatu vya Michezo vya Wilaya Unguja na Pemba sambamba na kuendeleza Siku ya Mazoezi ya Viungo kila ifikapo tarehe moja Januari ambapo hujumuisha vikundi vya mazoezi kutoka Unguja, Pemba na Dar-es-Salaam.

13. **Mheshimiwa Spika,** Maelezo zaidi ya mafanikio ya Wizara kwa mujibu wa Ibara za Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi cha miaka mitano 2015-2020 yanapatikana katika **Kiambatisho nambari 2.**

## 3.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilipanga kutekeleza programu kuu tatu kama zifuatazo: -
    i. Programu ya Maendeleo ya Vijana;
    ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
    iii. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.1 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

15. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikadiriwa kupokea **shilingi 9,691,200,000/=** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu. Kati ya fedha hizo **shilingi 5,691,200,000/=** kwa kazi za kawaida kati ya fedha hizo **shilingi 3,088,500,000/=** ni mishahara na **shilingi 2,602,700,000/=** ni kwa matumizi mengineyo. Katika utekelezaji wa kazi za maendeleo jumla ya **shilingi 4,000,000,000/=** zilitengwa ambapo jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=** zilipangiwa kutekeleza Programu ya Ajira kwa Vijana na **shilingi 2,000,000,000/=** ni kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 375,063,000/=**, kati ya hizo, **shilingi 255,063,000/=** ni makusanyo yanayoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na jumla ya **shilingi 120,000,000/=** ni makusanyo ya mirabaha. Kwa upande wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) ilipangiwa kukusanya **shilingi 230,000,000/=**, Baraza

la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) **shilingi 16,126,000/=** na Ofisi Kuu Pemba **shilingi 8,937,000/=**.

**Utekelezaji Halisi Kifedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

**17. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya **shilingi 3,849,652,582/=** zimepatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kazi za kawaida, sawa na asilimia **68** ya lengo la mwaka zilikadiriwa **shilingi 5,691,200,000/=**. Kwa upande wa mishahara jumla ya **shilingi 2,172,958,885/=** zilipatikana ambapo ni sawa na asilimia **70** ya lengo la mwaka ambapo zilikadiriwa **shilingi 3,088,500,000/=**. Kwa upande wa matumizi mengineyo jumla ya **shilingi 1,676,693,697/=** zimepatikana sawa na asilimia **64** ya lengo la mwaka ambapo zilikadiriwa **shilingi 2,602,700,000/=**.

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mishahara ya Idara zilizomo ndani ya Wizara, jumla **shilingi 2,009,833,870/=** sawa na asilimia **70** ya lengo la **shilingi 2,874,100,000 /=** zimepatikana. Kwa taasisi zinazopokea ruzuku, zilipata jumla ya **shilingi 163,125,105/=** ikiwa ni malipo ya mishahara ambapo ni sawa na asilimia **76** ya lengo la **shilingi 214,400,000/=**.

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi mengineyo, jumla ya **shilingi 1,214,716,214/=** zilipatikana kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na asilimia **67** ya lengo la **shilingi 1,800,400,000/=**. Vile vile, kwa taasisi zinazopata ruzuku zilipata jumla ya **shilingi 461,977,483/=** sawa na asilimia **58** ya lengo la **shilingi 802,300,000/=**.

**20. Mheshimiwa Spika,** makusanyo halisi ni jumla ya **shilingi 121,750,900/=** sawa na asilimia **48** ya lengo la mwaka kupitia Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) ilikusanya

**shilingi 113,875,900/=**, Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) **shilingi 1,239,500/=** na Ofisi Kuu Pemba **shilingi 6,635,500/=** ambazo ziliingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vile vile, **shilingi 142,373,067/=** sawa na asilimia **119** ambazo ni makusanyo ya mirabaha ya wasanii na wabunifu ikilinganishwa na lengo la **shilingi 120,000,000/=**.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za maendeleo zinazotokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=** zimepatikana sawa na asilimia **50** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

22. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshatumia **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya Programu ya Ajira kwa Vijana kutoka katika bajeti ya mwaka 2018/2019, hadi kufika Machi 2020.

23. **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa fedha zilizopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 na zilizopatikana hadi kufikia Machi 2020 umeainishwa katika **Kiambatisho Namba 1A hadi 1F.**

## 3.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2019/2020

### i. Programu ya Maendeleo ya Vijana

24. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,474,052,000/=**, kati ya fedha hizo, **shilingi 188,652,000/=** kwa mishahara, **shilingi 285,400,000/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 2,000,000,000/=** za utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya **shilingi 295,479,929/=** zilishapatikana sawa na asilimia **12** ya makadirio kati ya hizo **shilingi 122,428,180/=** ni mishahara na **shilingi 173,051,749/=** ni matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana***

25. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu Ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,474,052,000/=** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 295,479,929/=** sawa na asilimia **12** zilipatikana. ***(Tafadhali angalia kiambatanisho namba 1F NA 1E).***

26. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuyawezesha makundi ya vijana kiuchumi katika nyanja za kilimo, uvuvi, ushonaji na ufugaji, kutoa elimu ya uzalendo kwa vijana, kuratibu shughuli za mwenge wa uhuru, kuyawezesha mabaraza ya vijana katika fursa za kiuchumi pamoja na kutembelea na kusaidia vikundi vya vijana vya Unguja na Pemba.

**27. Mheshimiwa Spika,** vikundi vya vijana 17 vya kiuchumi vikiwemo vikundi vya ushonaji, ufugaji na kilimo viliwezeshwa kwa kupatiwa vifaa mbalimbali. Wizara imefanya ufuatiliaji wa vikundi vya kiuchumi vya vijana na jumla ya vikundi 50 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba vilifuatiliwa. Ziara hizo zilikuwa na lengo la kubaini shughuli zao za kiuchumi, mafanikio na changamoto zinazowakabili na kupewa ushauri wa kitaalamu.

**28. Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya uzalendo na stadi za maisha kwa vijana yametolewa ambapo jumla ya vijana wa kike 217 walipatiwa mafunzo ya uzalendo pamoja na kuhamasishwa kushiriki nafasi mbalimbali za uongozi. Aidha, mafunzo ya afya ya uzazi kwa vijana kama moja ya kipengele cha mafunzo ya stadi za maisha yametolewa ambapo jumla ya vijana 185 wakiwemo wanawake 100 na wanaume 85 kutoka Wilaya 5 za Unguja na Wilaya 3 za Pemba wamefaidika na mafunzo hayo.

**29. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Vijana la Zanzibar liliendesha mafunzo ya uandishi wa miradi kwa Vijana 33 kutoka katika Mabaraza ya Vijana ya Wilaya. Vijana hao walijifunza namna ya uandishi wa miradi pamoja na jinsi ya kuiendeleza miradi ambayo tayari imeshaibuliwa ili iwe endelevu. Aidha, vijana hao wanatumika katika kutayarisha maandiko mbalimbali ya miradi ya vijana wa maeneo mbalimbali pamoja na kuwafundisha vijana wenzao .

**30. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha Baraza la Vijana Zanzibar kiutendaji, maafisa wawili (2) wameshiriki mafunzo ya ujasiriamali Nchini China na mafunzo ya uchambuzi wa bajeti “Budget Analysis” yaliyofanyika Tanzania Bara. Aidha, mtendaji mmoja alishiriki Tamasha la Vijana wa Afrika na China lililofanyika nchini China kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kukuza ushirikiano wa Baraza la Vijana Zanzibar na taasisi zenye malengo yanayofanana.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kukuza na kuendeleza uzalendo kwa Vijana, Wizara kupitia Baraza la Vijana Zanzibar limewawezesha baadhi ya viongozi kutoka Mabaraza ya Vijana ya Wilaya na viongozi wa Baraza la Vijana la Zanzibar kushiriki katika Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizofanyika tarehe 14 Oktoba, 2019 Mkoani Lindi, lengo ni kuwajenga vijana wa mabaraza kuwa wazalendo kwa nchi yao kupitia matukio ya Kitaifa.

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa mwaka 2019, ambapo uzinduzi ulifanyika Mkoa wa Songwe mwezi Aprili, 2019, Mgeni rasmi alikuwa **Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan.** Aidha, kilele na kumbukumbu ya Baba wa Taifa na Wiki ya Vijana Kitaifa ilifanyika Mkoa wa Lindi. Mgeni rasmi katika kilele hicho alikuwa **Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli** na ujumbe wa mwenge kwa mwaka 2019 ulikua **''Maji ni Haki ya Kila Mtu, Tutunze Vyanzo Vyake na Tukumbuke Kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa''.**

33. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Vijana 1,200 walijiunga na Mabaraza ya Vijana na kufanya idadi ya wanachama kuongezeka kutoka 16,340 mwaka 2018- 2019 na kufikia 17,540 katika mwaka 2019 -2020 kati ya hao wanaume ni 8,351 na wanawake ni 9,189.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana Duniani kwa kufanya mdahalo wa wazi ambapo vijana wasiopungua 675 (wanaume 306 na wanawake 369) kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba walishiriki na kutoa maazimio yakiwemo vijana kupata nafasi ya kushiriki katika maadhimisho yote ya Kitaifa, kushiriki na kushirikishwa katika ngazi mbalimbali za maamuzi, kuendelea kuwathamini na kuwaheshimu Viongozi mbalimbali wa Kitaifa pamoja na kujadili utekelezaji na mipango kazi kwa kila Baraza la Vijana la Wilaya.

### *i. Programu ya Ajira kwa Vijana*

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ajira kwa Vijana inatekelezwa ndani ya programu ndogo ya Maendeleo ya Vijana. Itakumbukwa kwamba Serikali ilianzisha Programu ya Ajira kwa Vijana na kuidhinishia jumla ya **shilingi 3,000,000,000/=** kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hadi kumalizika kwa bajeti ya fedha mwaka 2018/2019 Wizara ilishaingiziwa jumla **shilingi 1,000,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo. Kwa kuwa Serikali iliahidi kuipatia Wizara fedha zilizobakia. Mnamo Julai 2019, jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=** ziliingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kuwezesha Wizara kuendelea kutekeleza shughuli ilizojipangia katika programu hiyo. Hadi kufikia Machi, 2020 fedha zote hizo zimeshatumika kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

36. **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Ajira kwa Vijana inatekelezwa kupitia vipengele vitatu (3) vikubwa ambapo ndani yake kuna maeneo madogo madogo, maeneo hayo ya programu ni kama yafuatayo:-

**a. Miradi ya kilimo**

i. Ukulima wa mboga kwa kutumia mahema “Green house”;
ii. Kusaidia vijana ufugaji wa kuku, nyuki na samaki; na
iii. Kilimo cha pilipili.

**b. Miradi ya viwanda**

i. Kuanzisha viwanda vidogo vidogo na vya kati vya mbao, utengenezaji bidhaa za chuma na “alluminium” pamoja na uchongaji;
ii. Kujenga na kuipatia vifaa Nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe; na
iii. Kuanzisha vituo vya ushoni na kutoa vifaa na nyenzo kwa vikundi vya vijana vya ushoni.

**c. Mradi wa kuwajengea uwezo vijana.**

i. Programu ya kutoa mafunzo kazi kwa vijana na mabaraza ya vijana; na

ii. Mradi wa kuibuwa na kukuza vipaji vya michezo.

**37. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji halisi wa Programu ya Ajira kwa Vijana hutokana na fedha zilizopatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa bajeti ya mwaka 2018/2019 ni kama ifuatavyo:-

**a) Mradi wa Kilimo**

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa awamu ya kwanza jumla ya vikundi 23 vya kilimo vyenye jumla ya vijana 507 ( 256 wanawake na 251 wanaume) vimenufaika na pembejeo mbalimbali za kilimo zikiwemo treya za miche, mbegu, mbolea, mipira ya kusambazia maji na matangi ya maji. Ambapo vikundi 16 kutoka unguja vyenye jumla ya vijana 339 ( 177 wanawake na 162 wanaume) na vikundi saba (7) kutoka Pemba vyenye jumla ya vijana 168 ( 79 wanawake na 89 wanaume).

**39. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa vitalu nyumba "Green house" 19 (Unguja 10 na Pemba 9) na uchimbaji wa visima 32 (Unguja 14 na Pemba 18) pamoja na miundombinu ya umwagiliaji maji unaendelea katika Wilaya za Unguja na Pemba. Jumla ya vitalu nyumba 13 na visima 27 kwa Unguja na Pemba vimeshakamilika na jumla ya vijana 991 watanufaika na kilimo hiki cha mahema kati ya hao vijana 581 kutoka Unguja na vijana 410 kutoka Pemba. Kazi hii inafanywa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatarajia kujenga na kuyafanyia ukarabati maeneo ya ufugaji ya vijana katika shughuli za ufugaji kuku, nyuki na samaki maeneo hayo ni Kinduni, Mkadini, Mwera, Maungani, Kidimni na Kitogani jumla ya vijana 176 watanufaika ambapo shughuli za uimarishaji wa maeneo ya ufugaji yanatarajiwa kuanza.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi wa pilipili itakumbukwa kwamba mradi huu ulianza lakini kwa bahati mbaya ulikabiliwa na changamoto mbalimbali hali iliopelekea wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuhoji ufanisi wa mradi huu. Baada ya hoja hizo Serikali iliunda tume ya wataalamu kwa madhumuni ya kufanya tathmini ya kina katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuangalia hali ya sasa, changamoto ziliopo na hatimae kutoa ushauri kwa Serikali ili kuleta ufanisi kwenye mradi huu.

42. **Mheshimiwa Spika,** tayari ripoti hiyo imewasilishwa Serikalini na Serikali imeshatowa maagizo kwa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Biashara na Viwanda na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Pamoja na mambo mengine yaliopo kwenye maagizo hayo ni:-

i. Mradi wa pilipili usimamiwe na Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na shirika la ZSTC kwa ajili ya kupata ushauri wa kitaalamu wa kilimo na masoko. Aidha, fedha za mradi zilizobakia ambazo ni jumla **Shillingi 376, 462, 104/=** zirejeshwe Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa utekelezaji;

ii. Kuangalia upya makubaliano yaliokuwepo ya mkataba kati ya ZSTC, "Kampuni ya Vegrab Organic Farming Limited" na vijana; na

iii. Kuhakikisha pilipili zinalimwa kwenye maeneo ambayo yamethibitishwa kitaalamu na taasisi zetu za kilimo Zanzibar.

**b) Miradi ya viwanda vidogo vidogo**

43. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya vikundi 21 vya ushonaji ( 12 Unguja na 9 Pemba ) vimepatiwa vifaa vya ushonaji katika awamu hii ya kwanza ambapo jumla ya vijana 330 ( 296 wanawake na 34 wanaume) wamepatiwa vifaa hivyo vikiwemo vyarahani vya batterfly, Singer, juki, pasi, mikasi na meza. Aidha, jumla ya vikundi vya vijana

132 (48 Pemba na 84 Unguja) wanaoendelea na mafunzo katika Vyuo vya Amali Unguja na Pemba watapatiwa vifaa vya ushonaji, uchongaji na uchomaji wa vyuma baada ya kuhitimu mafunzo kazi.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uimarishaji wa Nyumba ya Sanaa Wizara tayari imeshatangaza tenda kwa ajili ya kupata mkandarasi wa ujenzi wa nyumba hiyo ambapo itasaidia vijana katika eneo la Sanaa kupata mafunzo kazi na kuzalisha kazi za sanaa na utamaduni ambazo zitaweza kuuzika katika soko la utalii ndani na nje ya nchi.

**c) Mradi wa kuwajengea uwezo vijana**

45. **Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulihusisha mafunzo kazi maalumu (Tailor made course) katika fani ya ushoni, useremala na uchomaji (Welding), kuwapatia mafunzo vijana katika sanaa ya muziki, uigizaji, upambaji na uchoraji wa mwili na kuibuwa na kukuza vipaji vya wanamichezo mbalimbali.

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mafunzo maalumu kwa vijana jumla ya vijana 660 kati ya hao 420 kutoka Unguja na 240 kutoka Pemba mgawanyo huu umezingatia kiwilaya hivyo kila Wilaya imepewa nafasi ya vijana 60. Vijana hao wanaendelea na mafunzo kazi katika vyuo ya Amali Mkokotoni, Vitongoji, Mwanakwerekwe pamoja na Jeshi la Polisi Ziwani. Mafunzo hayo yanatolewa kwa fani ya Ushonaji, Uchongaji pamoja na uchomaji wa vyuma (Welding). Kiujumla vijana walitarajiwa kumaliza mnamo mwezi wa Mei mwaka huu lakini kutokana na tatizo la maradhi ya corona, vyuo vyote nchini vimefungwa lakini kwa sasa vijana hawa wanaendelea na mafunzo kwa vitendo (field) katika maeneo waliopangiwa na vyuo.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwenye eneo la kuibuwa na kukuza vipaji vya michezo, Wizara tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na baadhi ya vituo vya michezo (sports Academy)

vilivyopo pamoja na kamati ya Olimpic Tanzania (TOC) imeanza na inaendelea na shughuli za kuibuwa na kukuza vipaji pamoja na kuimarisha maeneo ya akademia kwa kuwapatia vifaa, taaluma na mahitaji mbalimbali.

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kwa kukisaidia kituo cha michezo cha JKU (JKU Sports Academy) kwa kukipatia vifaa vya michezo, vitanda, magodoro na kugharamia gharama mbalimbali za vijana waliopo kwenye kituo hicho na vijana 130 wanafaidika na programu hiyo wakiwemo wachezaji mpira na waamuzi wadogo. Aidha, Wizara imekisaidia kituo cha michezo cha Dole (Dole Sports Academy) kwa kukipatia vifaa vya michezo, "projector", "computer" na "photocopy" kwa ajili ya kufundishia ambapo vitasaidia vijana 157 waliokuwepo katika kituo hicho katika suala zima la kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo.

**d) Kusaidia vikundi vya Watu Wenye Ulemavu na Wenye Mahitaji Maalumu.**

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekabidhi vifaa vya kilimo, bajaji, mali ghafi za kutengenezea sabuni, mali ghafi za kutengenezea viatu, vyarahani, mashine za maji, waya wa fensi na matangi ya maji kwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa ajili ya vikundi 31 Unguja na Pemba vya Watu Wenye ulemavu. Lengo ni kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kuweza kujiajiri, ambapo vijana 607 watanufaika kwa awamu ya kwanza.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu ya Ajira kwa Vijana ilipangiwa jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=**. Wizara imeshawasilisha maombi ya fedha hizo ambapo jumla ya **shilingi 1,000,000,000/=** zitatumika kwa ujenzi wa Nyumba ya Sanaa, jumla ya **shilingi 500,000,000/=** zitatumika kusaidia vikundi vya vijana vya kilimo, ufugaji, uchongaji, ushonaji na uchomaji wa vyuma, jumla ya **shilingi 150,000,000/=** zitatumika

kusaidia miundombinu ya michezo ya kituo cha michezo cha Dole, jumla ya **shilingi 200,000,000/=** zitatumika kwa ununuzi wa boti kwa vijana na jumla ya **shilingi 150,000,000/=** zitatumika katika kuwapatia mafunzo kazi kwa vijana.

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha taratibu zote zikiwemo upatikanaji wa mkandarasi kwa Nyumba ya Sanaa na ujenzi wa miundombinu ya kituo cha michezo cha Dole ambapo itawezesha vijana kupata mafunzo kazi ya sanaa na kuzalisha bidhaa za kazi ya sanaa na kuendeleza uibuwaji wa vipaji vya michezo kwa vijana. Vile vile, ununuzi wa vifaa kazi kwa vijana, ununuzi wa boti kwa vijana wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi na utalii na kuwapatia mafunzo kazi vijana ili kuweza kujiajiri kupitia Vyuo vya Amali. Taratibu hizi zilichelewa kidogo kutokana na tatizo la janga la korona ambapo shughuli nyingi za kiuchumi zilisimama duniani na hapa kwetu Zanzibar hali iliopelekea kupunguza kasi ya utekelezaji wa shughuli za manunuzi.

**52. Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa vikundi vya vijana walionufaika na programu ya Ajira kwa vijana kwa awamu ya kwanza tafadhali angalia **kiambatanisho nambari 3A hadi 3D**

**ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo;**

**53. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 5,062,643,000/=** kati ya hizo **shilingi 1,715,743,000/=** ni mishahara na **shilingi 1,346,900,000/=** ni matumizi mengineyo, na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 4,145,127,854/=** sawa na asilimia **82** zilipatikana kati ya hizo **shilingi 1,189,434,115/=** ni mishahara, **shilingi 955,693,739/=** ni matumizi mengineyo na **shilingi 2,000,000,000/=** ni mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

**54. Mheshimiwa Spika,** programu hii inaundwa na programu ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo.

***Programu Ndogo 1: Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa***

**55. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa inaundwa na taasisi zifuatazo: Idara ya Utamaduni na Sanaa, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, (BASSFU), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (COSOZA).

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, programu hii ndogo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,542,643,000/=** kwa kazi za kawaida. Kwa upande wa mapato, ilikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 255,063,000/=**, hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 1,684,115,182/=** sawa na asilimia **66** zilizopatikana na kufanikiwa kukusanywa jumla ya **shilingi 121,750,900/=** sawa na asilimia **48**. **(Tafadhali angalia Kiambatanisho Namba 1A na 1E).**

**57. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuandaa matamasha ya utamaduni na kusaidia vikundi vya utamaduni, kukuza na kuendeleza Lugha ya Kiswahili, kuwapatia mafunzo wasanii na wabunifu, kuimarisha vikundi vya sanaa vya Taifa, kufanya udhibiti na ukaguzi wa kazi za sanaa pamoja na kusajili, kusimamia na kulinda kazi na haki za wasanii na wabunifu.

**58. Mheshimiwa Spika,** katika kulinda na kuendeleza utamaduni wa Mzanzibari Wizara ilifanikisha kufanyika kwa tamasha la 24 la

utamaduni wa Mzanzibari Unguja na Pemba. Tamasha hili lilishirikisha shughuli mbalimbali za kiutamaduni zikiwemo, ngoma za kiasili kutoka wilaya zetu za Unguja na Pemba, maonesho ya vyakula, kazi na bidhaa za kiutamaduni taarab asilia, maulidi ya homu, mchezo wa ngo'mbe na resi za ngalawa. Aidha, Wizara iliratibu juu kufanyika kwa matamasha tisa ya kijamii yanayokuza na kuendeleza utamaduni na utalii wa ndani.

59. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kukipatia vifaa vya muziki kikundi cha Taifa cha Taarabu kwa lengo la kukiwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi pamoja na kuwawezesha wasanii na wajasiriamali wa kazi za sanaa 110 kushiriki katika Tamasha la Kimataifa la JAMAFEST lililofanyika Tanzania Bara pamoja na wasanii **78** kushiriki katika matamasha ya Kitaifa yaliyofanyika ndani ya Zanzibar. Aidha, wafanyakazi wanne wa Nyumba ya Sanaa wamejengewa uwezo juu ya masomo ya lugha za alama kwa lengo la kutoa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika masomo ya sanaa.

60. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuandaa kongamano la Tatu la Kiswahili na maonesho ya vitabu vya Lugha ya Kiswahili ambalo liliwashirikisha wataalamu 250 kutoka nchi mbalimbali ikiwemo China, Uganda, Kenya, Japan, Burundi, Rwanda, Misri, Sweden, Austria, Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, imewawezesha watendaji wa Baraza la Kiswahili kushiriki katika makongamano ya Kiswahili ya Kimataifa yaliyoandaliwa na vyama na taasisi mbalimbali kama vile Chama cha lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), JAMAFEST, maonesho ya nchi za SADC na Tamasha la Utamaduni Pemba. Baraza la Kiswahili Zanzibar limeshirikishwa katika uandaaji wa waraka wa pendekezo lililotumika kushawishi kutumika kwa lugha ya Kiswahili katika mikutano ya SADC.

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuanzisha kanzi data ya wataalamu wa Kiswahili waliopo Zanzibar ambapo jumla ya

wataalamu wa Kiswahili 445 tayari wamesajiliwa katika kanzi data hiyo wakiwemo Wataalamu 14 wenye kiwango cha Uzamivu, 235 kiwango cha Shahada ya Pili na 194 Shahada ya kwanza. Lengo la kuanzishwa kwa kanzi data hiyo ni kuwatambuwa wataalamu wa Kiswahili waliopo Zanzibar.

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutangaza machapisho ya Kiswahili ndani na nje ya Zanzibar ambapo jumla ya machapisho 17 yameuzwa yakiwemo Kamusi la lahaja ya Kitumbatu, Jarida la Jahazi, Jarida maalumu la Kongamano, vitabu vya Matamko ya Msamiati, Kitabu cha Mawasiliano ya Msingi ya Kiswahili kwa Wageni, kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari. Vile vile, Baraza linaendelea kutoa huduma za Maktaba kwa wanafunzi kutoka Skuli na Vyuo Vikuu vya Zanzibar na Tanzania Bara. Jumla ya wanafunzi waliohudhuria 70 wakiwemo wanawake 27 na wanaume 43.

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikisha kuandaa mkutano kati ya **Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein** na wasanii wa fani mbalimbali za sanaa kutoka Unguja na Pemba kwa ajili ya kujadili changamoto na maendeleo ya sanaa nchini. Jumla ya wasanii 600 walishiriki katika mkutano huo. Aidha, Wizara imefanikiwa kutoa elimu juu ya nidhamu ya mavazi na umuhimu wake katika kudumisha haiba na maadili ya jamii ya Zanzibar.

64. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya kazi za sanaa 581 zimekaguliwa na kufanyiwa uhakiki kwa ajili ya kutolewa makosa na maelekezo ili ziweze kutumika hadharani kupitia Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni ambapo maonesho ya jukwaani 56, filamu 375 na maduka 150 ya filamu Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya vikundi 40 vya sanaa na utamaduni vimesajiliwa upya kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) ya mwaka 2015.

65. **Mheshimiwa Mwenyeki,** katika kupunguza uharamia wa hakimiliki, Wizara kupitia Afisi ya hakimiliki imefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya watumiaji wa kazi za sanaa. Watumiaji 256 wa kazi za hakimiliki kibiashara wamekaguliwa wakiwemo wenye maduka ya kuuza na kukodisha kazi za vinasa sauti vya kusikia na kuona (180), Mahoteli (75) Kumbi za Burudani (1). Aidha, watumiaji hao walielimishwa juu ya matumizi sahihi ya kazi za hakimiliki, kuepuka uharamia na umuhimu wa kulipia mirabaha ili waweze kufanya biashara zao kihalali.

66. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya kazi za hakimiliki 699 sawa na asilimia 200 ya makadirio ya usajili zimesajiliwa katika utaratibu wa kawaida wa kuingizwa katika mfumo wa kielekroniki kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na kuwa na takwimu ya kazi zilizosajiliwa na wafaidikaji wa mirabaha. Vile vile, Shirika la Milki Bunifu Ulimwenguni (WIPO) kupitia wataalamu elekezi waliwapatia mafunzo watendaji wa Ofisi, juu ya matumizi ya mfumo mpya wa Usajili "WIPO CONNECT" ambao unaweza kufikika na kutumika kwa mtumiaji akiwa eneo lolote kwani umetengenezwa kutumika katika mtandao (web based system).

67. **Mheshimiwa Spika,** katika kuifanya Zanzibar kuwa ni sehemu yenye kuheshimu masuala ya hakimiliki, Wizara kupitia Afisi ya hakimiliki imeandaa programu maalumu, ijulikanao kama ***"ZANZIBAR COPYRIGHT RESPECT JURISDCTION PROGRAM"*** kwa kuelimisha wanafunzi wa skuli za Msingi na Sekondari juu ya kuheshimu kazi za maandishi na kazi nyengine wakati wanapojifunza kuandika na kuchora kazi zao wenyewe kwa kufuata misingi ya hakimiliki. Programui hiyo imeanza kwa majaribu ambapo skuli 5 za Mkoa wa Mjini Magharibi za Msingi na Sekondari na umehitimishwa kwa wanafunzi walioshinda kukabidhiwa zawadi zao, na programu hio itaendelea tena kwa skuli za Msingi na Sekondari kwa Unguja na Pemba katika mwaka wa fedha 2020/2021.

**68. Mheshimiwa Spika,** wabunifu na wasanii wagonjwa 25 wamefikiwa katika maeneo yao kwa Unguja na Pemba, na kuwapatia msaada unaotokana na eneo maalumu la mirabaha. Vile vile, wasanii 50 wamefikiwa kwa Unguja na Pemba, kwa lengo la kuwaelimisha juu ya umuhimu wa ulinzi wa kazi na usajili wa kazi zao. Aidha, migogoro mitatu (3) ya uvunjwaji wa hakimiliki imepokelewa ikiwemo mgogoro mmoja wa kazi za maandishi na migogoro miwili (2) ya muziki wa kizazi kipya. Migogoro yote hiyo inaendelea kufanyiwa kazi ili kupatiwa ufumbuzi stahiki.

**69. Mheshimiwa Spika,** mirabaha yenye thamani ya **shilingi 142,373,067/=** ilikusanywa kutoka kwa watumiaji mbalimbali wakazi za hakimiliki kibiashara na zitagaiwa kwa wasanii na wabunifu 1,280 wa vikundi mbalimbali vya sanaa na ubunifu vikiwemo vikundi vya Taarab, Muziki wa Kizazi Kipya, Kasida, Muziki wa Injili, Filamu, Maigizo na Mawaidha. Aidha, Afisi imewasaidia wasanii wa vikundi mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli zao za kisanii, vikundi vyenyewe ni Chama cha Wasanii wa Muziki wa Kikazi Kipya na Swahili Media.

**70. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Michezo na Utamaduni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanikiwa kufanya mashindano ya uibuaji wa vipaji vya sanaa za maigizo na uchoraji. Fainali ya mashindano ya fani ya maigizo ilishirikisha skuli ya Ngwachani kutoka Pemba na Fujoni kwa Unguja ambapo mshindi wa fainali hiyo ni skuli ya Msingi Fujoni. Aidha, Sanaa ya uchoraji ilifanikiwa kuzikutanisha skuli ya Konde kutoka Pemba na skuli ya Mtoni kwa Unguja ambapo Mshindi wa fainali hiyo ni skuli ya Msingi Mtoni.

**71. Mheshimiwa Spika,** jumla ya vipindi 85 vimerushwa hewani vikiwemo 37 vinavyohusu elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuvisajili vikundi vya sanaa. Vipindi 12 kuhusu elimu ya masuala ya hakimiliki na vipindi 36 vya kuimarisha na kuendeleza matumizi

fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi. Vipindi vyote vimerushwa hewani kupitia televisheni ya “Zanzibar Cable”, ZBC TV na Redio, Chuchu FM, Coconut FM, Redio ya Umoja wa Mataifa na Zenj FM.

***Programu Ndogo 2: Uendeshaji na Ukuzaji wa Michezo***

72. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uendeshaji na Ukuzaji wa Michezo inatekelezwa na Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ). Kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,520,000,000/=** ambapo jumla ya **shilingi 520,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/=** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya **shilingi 2,461,012,672/=** zimepatikana kati ya hizo **shilingi 461,012,672/=** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **89** na jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=** sawa na asilimia **100** ni za utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. **(Tafadhali angalia Kiambatanisho Namba 1D).**

73. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuandaa mafunzo ya michezo ya Kitaifa na Kimataifa, kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya michezo, kusaidia timu za Taifa kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa na Kimataifa, kusaidia vyama vya Michezo na vilabu pamoja na kufanya mapitio ya sheria namba 5 ya mwaka 2010 ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

74. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuandaa na kusimamia mafunzo ya utawala na uongozi pamoja na mafunzo ya riadha kwa vyama mbalimbali vya michezo vikiwemo Chama cha Michezo cha Watu Wenye Mahitaji Maalumu Zanzibar (SOZ), Chama cha Michezo kwa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SAD’z) na Shirikisho la Michezo ya Viziwi Zanzibar (SHIMIVIZA). Jumla ya washiriki 70

(54 wanaume na 16 wanawake) walishiriki mafunzo hayo kutoka Unguja na Pemba. Mkufunzi wa Mafunzo hayo ni Mtaalamu kutoka Ujerumani kupitia jumuia ya Michezo ya "Land Sport Bunds".

75. **Mheshimiwa Spika,** katika uimarishaji wa viwanja vya michezo Zanzibar, Wizara imefanyia matengenezo makubwa Uwanja wa Amaan sehemu ya jukwaa la VIP, ukarabati wa vyoo kwa kuweka ukuta (partition), marekebisho ya mfumo wa maji, uwekaji wa milango ya vyoo, upakaji wa rangi ndani na nje pamoja na matengenezo ya taa.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza michezo nchini, Wizara imefanikiwa kusaidia vilabu na timu za Taifa mbalimbali kushiriki mashindano ya Kimataifa. **(Kiambatisho nambari 4 kinahusika).** Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar limefanikiwa kuviwezesha vyama vitatu vya michezo kuandaa na kushiriki katika mashindano ya ndani na Kitaifa. Miongoni mwa vyama hivyo ni Chama cha mchezo wa Riadha, Chama cha Basketball na Chama cha Judo.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa michezo ya Watu Wenye Ulemavu, Baraza limesaidia Shirikisho la Michezo ya Viziwi katika maandalizi ya kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika nchini Kenya.

78. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeweza kufanikisha marekebisho ya Sheria Namba 5 ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar na rasimu ya awali tayari imepatikana kwa ajili ya kupelekwa kwa wadau wa michezo ili kupata maoni yao.

### *i. Mradi wa Uimarisha wa Viwanja vya Michezo*

79. **Mheshimiwa Spika,** mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo unatekelezwa ndani ya programu ndogo ya uimarishaji na uendelezaji

wa michezo, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulipangiwa jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=**, na hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 2,000,000,000/=** zimepatikana sawa na asilimia **100.**

**80. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipanga kukiimarisha kiwanja cha Amaan kwa kununua ubao wa matangazo (scoreboard), ujenzi wa mkeka (base) pamoja na uwekaji wa nyasi bandia. Wizara imeshakamilisha hatua za awali za malipo kwa wahusika kinachosubiriwa ni kufika kwa vifaa vilivyoagizwa kutoka nje ya nchi na hatua za utekelezaji zianze rasmi.

### iii. Programu ya Uendeshaji na Mipango Katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**81. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020, programu hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 2,154,505,000/=** kati ya hizo **shilingi 1,184,105,000/=** ni mishahara na **shilingi 970,400,000/=** ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi 1,409,044,799/=** sawa na asilimia **65** zilipatikana kati ya hizo **shilingi 861,096,590/=** ni mishahara na **shilingi 547,948,209/=** ni matumizi mengineyo.

***Programu ndogo1: Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo***

**82. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,438,036,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2020, imefanikiwa kupata **shilingi 915,396,727/=** sawa na asilimia **64** ya fedha zilizopatikana. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

**83. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, shughuli zifuatazo

zilipangwa kutekelezwa; kuwajengea uwezo wafanyakazi, kuratibu shughuli za viongozi wa Wizara Kitaifa na Kimataifa, kutoa uelewa kwa wafanyakazi juu ya masuala mtambuka, kuimarisha mazingira bora ya kazi na kuandaa na kusimamia mpango wa manunuzi.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kukuza na kuimarisha utendaji wa kazi katika Wizara, Idara imeweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi watano (5) katika ngazi na fani tofauti. Aidha, wafanyakazi 173 wamepatiwa mafunzo ya ndani kuhusiana na upimaji wa utendaji kazi (Performance Appraisal), athari za rushwa kazini, utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa Umma, uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni zake, utayarishaji wa mpango wa urithishwaji wa madaraka na uigizaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kielectroniki (Data base). Mafunzo yote haya yalilenga kukuza na kuendeleza utendaji mzuri wa majukumu ya wafanyakazi ya kila siku.

85. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia shughuli za kikazi za Viongozi Wakuu wa Wizara katika taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa upande wa Pemba na Unguja, pamoja na taasisi mbalimbali zilizopo Dar- es- Salaam zinazofanyakazi kwa mashirikiano na Wizara yetu kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa Wizara. Lengo la ziara hizi ni kusimamia kwa ukaribu utendaji wa kazi katika taasisi hizo pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watendaji. Aidha, kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na wadau waliopo nje ya nchi, Idara imewawezesha watendaji wakuu wa Wizara kushiriki mikutano mbalimbali nchini Ufaransa, China na Kenya.

86. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake kiutendaji ya kila siku, Wizara imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuzipatia vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kazi kwa watendaji wake kwa ajili ya kuongeza bidii na kuimarisha ufanisi wa

kazi. Pia wafanyakazi wote wamepatiwa stahiki zao kama vile malipo baada ya saa za kazi, fedha za likizo, haki ya mapumziko baada ya kujifungua mtoto kwa mama na baba. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa rasilimali watu wa miaka mitano utakaomalizikia mwaka 2021/2022.

87. **Mheshimiwa Spika,** ili kuleta ufanisi mzuri wa matumizi ya rasimali fedha, Wizara imeweza kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ripoti za fedha na ukaguzi kwa kila robo mwaka kwa lengo la kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha za umma yanafanyika. Aidha, Wizara imeratibu mikutano mbalimbali ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi, mikutano ambayo imewezesha kuongeza ufanisi na kasi kubwa katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara.

***Programu ndogo 2: Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara***

88. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 160,400,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2020 imefanikiwa kupata jumla ya **shilingi 70,835,400/=** sawa na asilimia 44 ya fedha zilizopatikana. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E).**

89. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; Kuandaa mipango ya muda mfupi na mrefu ya Wizara, kufanya mapitio ya Sera, kuratibu na kusimamia tafiti za Wizara, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi na programu za Wizara na kuandaa bajeti ya Wizara.

90. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kutayarisha mpango wa mwaka wa utekelezaji, mpango wa ufuatiliaji na tathmini na kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika taasisi zinazo husika. Aidha, imetayarisha hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

91. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha kuifanyia tafsiri Sera ya Michezo kwa lugha ya Kiengereza ili kutoa fursa kwa wahusika wengi kuweza kutumia. Aidha, Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana na Sera ya Utamaduni imeshakamilika kwa ngazi za Wizara na inatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi za juu za maamuzi. Vile vile, utayarishaji wa Mpango wa Utekelezaji wa sera ya Utamaduni na Sera ya Maendeleo ya Vijana kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa sera hizo unaendelea.

92. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya utafiti wa matumizi ya vifaa vya kale kwa Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba. Jumla ya wananchi 552 wakiwemo watumiaji wa vifaa vya kale, wauzaji, maafisa utamaduni wa Wilaya na Masheha walishiriki kutoa maoni. Utafiti huo umegundua kuwa matumizi ya vifaa vya kale yamepunguwa kwa kasi kubwa, hasa Kiti cha Marimba, Hando na Gae la Manda, ripoti ya matokeo ya utafiti huo imeshawasilishwa kwa wahusika wa utamaduni. Vile vile, Wizara imeanza kufanya utafiti wa kuwatambua wanamichezo wa zamani waliofanya vizuri ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya wanamichezo wa zamani 300 watafikiwa.

93. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji miradi, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi iliyofuatiliwa ni Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya-Pemba, Kishindeni na Kangaani, kwa upande wa Unguja Mkokotoni, Kama na maeneo ya vijana kupitia Programu ya Ajira kwa Vijana.

94. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi Wizara imemuwezesha mtendaji kushiriki katika mafunzo ya muda mfupi nchini China. Vile vile, Wizara imeendelea kuratibu ziara za Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Unguja, Pemba na Dar-es-Salaam katika kufanya ufuatiliaji wa shughuli za taasisi zilizochini ya Wizara.

***Programu ndogo 3: Kuratibu na Kusimamia Utawala na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba***

95. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 556,069,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2020 imefanikiwa kupata jumla ya **shilingi 422,812,672/=** sawa na asilimia 76 ya fedha zilizopatikana. **(Tafadhali angalia kiambatisho namba 1D na 1E),**

96. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha programu hii inatekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, shughuli zifuatazo zilipangwa kutekelezwa; kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba, kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi Ofisi Kuu Pemba, kutoa uelewa kwa wafanyakazi katika kuimarisha utendaji kazi.

97. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kutoa huduma za kiutawala na za kiuendeshaji kwa kusimamia na kufuatilia Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya (Kiwanja cha Kishindeni kwa Wilaya ya Micheweni na Kiwanja cha Kangani kwa Wilaya ya Mkoani). Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa "Green House" na uchimbaji wa visima kwa miradi ya vijana, kusimamia zoezi la ugawaji wa vifaa kwa vikundi vya wajasiriamali vijana chini ya Programu ya Ajira kwa Vijana, kusimamia Tamasha la 24 la Utamaduni wa Mzanzibari pamoja na kusimamia shughuli za sanaa na wasanii kwa upande wa Pemba.

98. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanya mikutano ya wadau wa Wizara kama vile Wenyeviti na Makatibu wa vyama vya Michezo Pemba, Wenyeviti na Makatibu wa vikundi vya Sanaa mbalimbali wakiwemo wa Maigizo, Uchoraji, Ufumaji, vikundi vya Ngoma na Taarabu, Wenyeviti na Makatibu wa mabaraza ya vijana ya Shehia na Wilaya, kwa kushirikiana na Idara ya vijana imefanya mkutano na

wajasiriamali vijana. Mikutano hiyo ilikuwa na lengo la kujadiliana masuala yanayohusu vijana, sanaa na michezo kwa ujumla. Vile vile, jumla ya vikundi 25 vya sanaa na vikundi 32 vya wajasiriamali vijana vimetembelewa kwa Wilaya zote za Pemba kwa lengo la kujua mahitaji yao katika jitihada za kuviendeleza na kuvikuza vikundi hivyo ili vitoe ajira zaidi kwa vijana.

**99. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kutoa huduma za uendeshaji na utawala, jumla ya wafanyakazi watatu (3) (1 mwanaume na 2 wanawake) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu mmoja katika fani ya Ufuatiliaji na Tathmini ngazi ya shahada ya pili katika Chuo Kikuu Huria na wawili fani ya Uongozi wa rasilimali watu ngazi ya stashahada katika chuo cha Utawala wa Umma na ZCBE.

**100. Mheshimiwa Spika,** jumla ya wafanyakazi wanane (8) (3 mwanaume na 5 wanawake) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi katika Chuo cha Utawala wa Umma na wafanyakazi 20 (12 mwanaume na 8 wanawake) wamepatiwa mafunzo juu ya mpango wa manunuzi. Vile vile, matengenezo ya kiwanja cha Gombani, ununuzi wa vitendea kazi, kulipa stahiki za wafanyakazi huduma za maji na umeme navyo vimefanyika.

**101. Mheshimiwa Spika,** watendaji wa Ofisi Kuu Pemba wamefanya vikao mbalimbali vya wafanyakazi na vikao vya Kamati ya Uongozi vikiwa na lengo la kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kukumbushana haki na wajibu wa kila mfanyakazi. Aidha, kuratibu vikao na ziara za wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, zikiwemo kutembelea ujenzi wa "Green House" na ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya zimefanyika.

## 4.0. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo imepangiwa jumla ya **shilingi 10,890,500,000/=** kati ya fedha hizo **shilingi 6,390,500,000/=** kwa matumizi ya kawaida na **shilingi 4,500,000,000/=** kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za matumizi ya kazi za kawaida, jumla ya **shilingi 3,080,600,000/=** ni mishahara ambapo **shilingi 2,857,800,000/=** ni mishahara ya Idara zilizomo ndani ya Wizara na **shilingi 222,800,000/=**ni mishahara kwa taasisi zinazopokea ruzuku. Kwa upande wa matumizi mengineyo jumla ya **shilingi 3,309,900,000/=**, kati ya hizo matumizi mengineyo kwa Idara za Wizara ni jumla ya **shilingi 2,214,300,000/=** na kwa taasisi zinazopokea ruzuku ni jumla ya **shilingi 1,095,600,000/=.**

## 4.1. MAENEO YA VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021

104. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imejipangia maeneo muhimu ya utekelezaji kuwa ni vipaumbele kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo: -

i. Kuendeleza programu za kuwawezesha vijana kiuchumi, kujenga moyo wa uzalendo, ari ya kujitolea na kuimarisha mahusiano ya vijana ndani na nje ya nchi pamoja na programu za malezi bora;

ii. Kuendeleza programu za kukuza, kulinda, kuenzi na kudumisha utamaduni wa Mzanzibari

iii. Kuimarisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi ili kutumika kama bidhaa inayouzika na kuwa chanzo cha ajira;

iv. Kusimamia mageuzi ya sekta ya sanaa na ubunifu kuwa ni

uchumi kwa kuwapatia mafunzo na vifaa wasanii na wabunifu pamoja na kusimamia kazi zao ili kuhakikisha wanafaidika nazo na kuweza kuchangia katika ukuwaji wa pato la taifa;

v. Kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo pamoja na kuibua vipaji vya wanamichezo kwa kushirikiana na taasisi nyengine za michezo na vilabu binafsi; na

vi. Kufanya tafiti katika maeneo ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kukamilisha Sera ya Filamu na Sera ya lugha.

## 5.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KUBWA NA NDOGO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

105. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo itatumia jumla ya **shilingi 10,890,500,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu kama ifuatavyo: -

i. Programu ya Maendeleo ya Vijana ni **shilingi 2,521,115,000/=;**

ii. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ni **Shilingi 5,887,148,000/=**; na

iii. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni **shilingi 2,482,237,000/=**.

**(Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1F).**

## 1. Programu Kuu: PS0101 Maendeleo ya Vijana.

106. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii, ni kuratibu shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kuwawezesha vijana ili kuimarika kiuchumi, kijamii na kisiasa kupitia programu mbalimbali. Aidha, matokeo ya muda mrefu katika programu hii ni kuongeza idadi ya ajira kwa vijana kwa kuwawezesha kwa kuwajengea uwezo kupitia programu mbalimbali. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 2,521,115,000/=** na imepangiwa kusimamia programu ndogo moja: -

*i.* ***Programu Ndogo: SS010101 Maendeleo ya Vijana (shilingi 2,521,115,000/=)***

107. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya maendeleo ya vijana inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar ambapo jukumu la msingi katika Programu ndogo hii ni kuwawezesha vijana ili kuimarisha ustawi wao na kujenga uchumi na maendeleo ya jamii.

108. **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinazotolewa katika programu hii ndogo ni kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya vijana, kuandaa miongozo mbalimbali ya shughuli za maendeleo ya vijana, kuratibu shughuli za kizalendo na Mwenge wa Uhuru Kitaifa, kusimamia uendeshaji wa mabaraza ya vijana katika ngazi zote, kuyawezesha mabaraza ya vijana kiuchumi ili yajiendeleze na kukuza ajira kwa vijana.

109. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuendelea kuwasaidia vijana katika shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, kuwapitia mafunzo kazi, kuwapatia vifaa vya kufanyia kazi pamoja na uibuaji wa vipaji vya sanaa na michezo kupitia programu ya ajira kwa vijana;
ii. Kuyajengea uwezo na uzalendo Mabaraza ya Vijana ya Wilaya na vijana kwa ujumla ili kuongeza ari ya kujitolea, kuipenda nchi yao na kuwaheshimu viongozi wa kitaifa;
iii. Kuendelea kuwashirikisha na kuwaunganisha vijana na fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii Kitaifa na Kimataifa na kuendeleza miradi ya vijana kupitia programu mbalimbali zilizopo;
iv. Kuratibu shughuli za Mwenge wa Uhuru Kitaifa;
v. Kuwawezesha wajasiriamali katika kubuni mbinu za kujikwamua kiuchumi kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kutoa elimu juu ya afya ya uzazi na kuhamasisha vijana juu

ya upimaji wa VVU na kuwaunganisha vijana na program ya Jukwaa la Vijana kidijitali juu ya kupata taarifa mbalimbali na kutoa michango yao; na

vi. Kuendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia elimu ya stadi ya ujuzi na vifaa wafanyakazi ili kuleta ufanisi wa kazi.

110. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 2,521,115,000/=**ikiwa ni **shilingi 521,115,000/=** kwa kazi za kawaida na **shilingi 2,000,000,000/=**kwa utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana.

## 2. Programu Kuu: PS0102 Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

111. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa za Zanzibar zinaenziwa, pia wasanii wanaendelezwa kiuchumi ili kupunguza umasikini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga amani, utulivu, urafiki, ajira pamoja na kujenga afya kwa jamii. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa soko la kazi za sanaa, uhifadhi wa utamaduni, kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili na kukuza michezo. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 5,887,148,000/=**na itakuwa na programu ndogo mbili.

i. Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu ni **shilingi 2,609,948,000/=**; na

ii. Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo ni **shilingi 3,277,200,000 /=**.

ii. ***Programu Ndogo: SS010201 Uimarishaji, Uhifadhi na Uendeshaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu***

112. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu inatekelezwa na Idara na Taasisi zifuatazo: Idara ya Utamaduni, Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni, Baraza la Kiswahili Zanzibar na Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Jukumu la msingi katika programu ndogo ni kusimamia, kuratibu, kuimarisha, kuendeleza na kudumisha shughuli zote za utamaduni, sanaa na ubunifu Zanzibar.

113. **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotarajiwa kutolewa ni uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za utamaduni kwa wananchi, uendelezaji na ukuzaji wa shughuli za sanaa na wasanii, kurikodi kazi za sanaa kupitia Studio ya Filamu na Muziki, uratibu wa kazi za sanaa na wasanii, ukaguzi wa filamu na sanaa za maonesho, utoaji wa elimu kuhusu matumizi fasaha ya Kiswahili, usimamizi wa hakimiliki pamoja na ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wenye hakimiliki.

114. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu ndogo hii ili kufikia malengo yake shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuratibu na kusimamia maendeleo na uhifadhi wa utamaduni pamoja na kuviwezesha vikundi vya sanaa na utamaduni kushiriki katika matamasha ya Kitaifa na Kimataifa;
ii. Kuhamasisha na kuendeleza utumiaji sahihi wa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi, kwa kupitia mafunzo mbali mbali, matamasha, makongamano na mikutano ya Kimataifa ya Kiswahili;
iii. Kuendelea kuwajengea uwezo wasanii ili wainuke kiuchumi kwa kuwapatia mafunzo na utaalamu wa kutengeneza kazi za sanaa na ubunifu kwa maendeleo ya kijamii, kiutamaduni na uchumi;

iv. Kuendeleza programu ya ukuzaji wa sanaa kwa kuibua vipaji kwa wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari, vijana, pamoja na vikundi vya kijamii ili kuwajengea msingi imara katika shughuli za sanaa;
v. Kufanya ukaguzi wa kazi za sanaa nchini katika kulinda na kuhifadhi mila, silka na maadili ya Zanzibar;
vi. Kusimamia na kuimarisha ukusanyaji mirabaha kwa kazi za sanaa na kazi za maandishi pamoja na kupambana na uharamia wa hakimiliki katika kulinda maslahi ya wasanii nchini; na
vii. Kuendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kuwapatia elimu na vifaa wafanyakazi ili kuleta ufanisi wa kazi.

115. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 2,609,948,000/=** kwa kazi za kawaida na makusanyo jumla ya **shilingi 228,141,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vile vile, makusanyo ya **shilingi 150,000,000/=** ambazo hukusanywa na taasisi ya Hakimiliki kwa ajili ya mirabaha ya wasanii na wabunifu.

***iii. Programu ndogo: SS01010202 Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo***

116. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya ukuzaji na uendelezaji wa michezo inatekelezwa na Idara na Taasisi zifuatazo: Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar. Jukumu kuu la programu ndogo ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa nchini. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu na uendelezaji wa shughuli za michezo, uendelezaji wa miundombinu ya michezo na usimamizi wa shughuli za vyama vya michezo kupitia Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar.

117. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii itekelezeke kwa ufanisi, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: -

i. Kuanzisha, kuimarisha na kuendeleza vituo vya michezo (Sports Academy) kwa ajili ya kuibua vipaji pamoja na kuandaa matamasha ya michezo kwa kushirikiana na taasisi na vilabu binafsi;

ii. Kusaidia timu za Taifa, vilabu na Vyama vya Michezo kushiriki na kuandaa mashindano ya Kitaifa na Kimataifa;

iii. Kuandaa mashindano ya mawizara, mashirika na taasisi za Serikali;

iv. Kuwasaidia viongozi wa vyama vya michezo, waamuzi na makocha kushiriki mafunzo ya Kitaifa na Kimataifa; na

v. Kuimarisha uwanja wa Amaani, Gombani, Mao- Zedong na Viwanja vya Wilaya.

118. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 3,277,200,000/=** ambapo **shilingi 777,200,000/=** kwa kazi za kawaida na jumla ya **shilingi 2,500,000,000/=** kwa kazi za maendeleo ambazo ni za utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo.

**3. Programu Kuu: PS0103 Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.**

119. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia utawala na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa usimamizi bora wa mipango na uendeshaji wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **shilingi 2,482,237,000/=** na itasimamia programu ndogo tatu.

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara ni **Shilingi 170,000,000/=**;

ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni **Shilingi 1,473,725,000 /=**; na
iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba ni **Shilingi 838,511,000/=.**

**i. Programu Ndogo: SS010301 Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**.

**120. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia mipango mikuu ya Wizara ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera na utafiti, kuratibu na kuandaa bajeti ya Wizara, kuandaa mipango ya muda mfupi na mrefu ya Wizara pamoja na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya Wizara.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii kwa ufanisi shughuli zifuatazo zinatarajiwa kutekelezwa: -

i. Kuchapisha Sera ya Maendeleo ya vijana, Sera ya Utamaduni pamoja na ukamilishaji wa Sera ya Filamu na Sera ya Lugha ya Kiswahili;
ii. Kuratibu na kusimamia tafiti za Wizara katika sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
iii. Kuandaa bajeti, mipango ya Wizara na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na programu za Wizara;
iv. Kuimarisha mazingira bora ya kazi pamoja na huduma, vifaa na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ya Mipango; na
v. Kuendelea kuratibu vikao vya SMT na SMZ kwa Wizara na taasisi zilizomo chini ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**122. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 170,000,000/=** kwa kazi za kawaida.

ii. **Programu Ndogo: SS010302 Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

123. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la kusimamia shughuli zote za utawala, utumishi, maendeleo wajibu na maslahi ya wafanyakazi wa Wizara.

124. **Mheshimiwa Spika,** lengo mahususi la programu hii ndogo ni usimamizi na uendeshaji mzuri wa wafanyakazi wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni kujenga uwezo kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wote na usimamizi wa mpango wa manunuzi na utekelezaji wa bajeti.

125. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2020/2021, Idara kupitia programu ndogo hii inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia fursa za mafunzo ya muda mfupi na mrefu pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya uelewa hasa katika masuala mtambuka ikiwemo udhalilishaji wa kijinsia, ukimwi pamoja na mikakati ya kupambana na rushwa na athari za rushwa katika utoaji wa huduma kwa jamii;

ii. Kuendelea kufanya upimaji wa utendaji kazi wa wafanyakazi kwa lengo la kuongeza ufanisi mzuri wa kazi;

iii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango wa manunuzi na mpango wa matumizi ya fedha kwa ajili ya kuwa na utaratibu mzuri ambao utafuatwa na taasisi zote zilizo chini ya Wizara;

iv. Kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa haraka; na

v. Kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

126. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 1,473,725,000/=** kwa kazi za kawaida.

**iii. Programu Ndogo: SS010303 Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.**

127. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia utawala, uendeshaji na mipango inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Programu ndogo hii ina jukumu la kuhakikisha mipango, malengo na shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

128. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo ni kusimamia na kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni uratibu wa sera, tafiti na mipango mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu miradi ya maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

129. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zinatarajiwa kutekelezwa: -

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba;
ii. Kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi wafanyakazi wa Ofisi Kuu Pemba;
iii. Kutoa uelewa kwa wafanyakazi kuhusiana na masuala mbalimbali katika kuimarisha utendaji kazi;

iv. Kusimamia shughuli za miradi inayotekelezwa Pemba; na
v. Kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiutendaji za Wizara zinazofanyika Unguja na nje ya Zanzibar.

**130. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **shilingi 838,511,000/=** kwa kazi za kawaida.

## 6.0 SHUKRANI

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa kumaliza hotuba yangu naomba kutoa shukurani zangu za dhati na za kipekee kwa **Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** kwa kuniteuwa kuwa miongoni mwa Mawaziri katika Baraza la Mapinduzi kwa kipindi hiki cha awamu ya pili cha uongozi wake.

**132. Mheshimiwa Spika,** nawapongeza na kuwashukuru Mawaziri na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia kwa kipindi chote tulichokuwa Barazani katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku kwa mujibu wa Sheria. Michango, maoni, ushauri na hoja mbali mbali walizoziwasilisha zilisaidia sana katika kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Wizara na naamini michango hiyo ilikuwa na nia ya kujenga na sio kubomoa

**133. Mheshimiwa Spika,** kwa udhati kabisa naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Bi. Lulu Msham Abdalla, Katibu Mkuu Nd. Omar Hassan Omar, Naibu Katibu Mkuu Nd. Amour Hamil Bakari, Makatibu Watendaji, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wote pamoja na Wenyeviti na wajumbe wa bodi zilizochini ya Wizara kwa jitihada wanazozichukuwa za kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake iliojipangia kwa ufanisi mkubwa.

134. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuzishukuru taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali kwa kushirikiana na Wizara katika kufanyakazi kwa pamoja na kuhakikisha majukumu tuliyopewa yanatekelezeka kama ilivyopangwa na kwa ufanisi katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, shukrani zaidi kwa vyombo vyetu vya habari vya Serikali na binafsi kwa ushirikiano mkubwa tulionao katika kuwajuulisha wananchi taarifa zinazotokana na Wizara yetu.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021.

135. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya **shilingi 10,890,500,000/=**. Kati ya hizo **shilingi 6,390,500,000/=** kwa kazi za kawaida, **shilingi 4,500,000,000/=** kwa utekelezaji miradi ya Wizara ambapo **shilingi 2,000,000,000/=** kwa Programu ya Ajira kwa Vijana na **shilingi 2,500,000,000/=** kwa Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato ya **shilingi 228,141,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia, makusanyo ya mirabaha ya **shilingi 150,000,000/=.**

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nawaomba wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie bajeti hii ya Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

137. **Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja

**BALOZI ALI ABEID KARUME (MBM),**
**Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**
**Zanzibar.**

# VIAMBATANISHO

**VIAMBATISHO**
**KIAMBATISHO NAMBA 1 A**
**FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA**
**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULY -MARCH 2019/2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 376,069,000 | 306,147,690 | 81% |
| | | Matumizi Mengineo | 180,000,000 | 116,664,982 | 65% |
| | **JUMLA** | | **556,069,000** | **422,812,672** | **76%** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 160,400,000 | 70,835,400 | 44% |
| | **JUMLA** | | **160,400,000** | **70,835,400** | **44%** |
| 3 | Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 808,036,000 | 554,948,900 | 69% |
| | | Matumizi Mengineo | 630,000,000 | 360,447,827 | 57% |
| | **JUMLA** | | **1,438,036,000** | **915,396,727** | **64%** |
| 4 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 188,652,000 | 122,428,180 | 65% |
| | | Matumizi Mengineo | 120,000,000 | 74,553,500 | 62% |
| | **JUMLA** | | **308,652,000** | **196,981,680** | **64%** |
| 5 | Idara ya Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,501,343,000 | 1,026,309,100 | 68% |
| | | Matumizi Mengineo | 290,000,000 | 207,216,833 | 72% |
| | **JUMLA** | | **1,791,343,000** | **1,233,525,933** | **69%** |
| 6 | Idara ya Michezo | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 420,000,000 | 384,997,672 | 92% |
| | **JUMLA** | | **420,000,000** | **384,997,672** | **92%** |
| | **Jumla ya Mishahara** | | **2,874,100,000** | **2,009,833,870** | **70%** |
| | **Jumla ya Matumizi Mengine** | | **1,800,400,000** | **1,214,716,214** | **67%** |
| | **Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **4,674,500,000** | **3,224,550,084** | **69%** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **TAASISI ZA RUZUKU** | | | | |
| 1. | Baraza la Vijana Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 165,400,000 | 98,498,249 | 60% |
| | | | **165,400,000** | **98,498,249** | **60%** |
| 2. | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | Mishahara | 214,400,000 | 163,125,015 | 76% |
| | | Matumizi Mengineo | 288,000,000 | 89,128,816 | 31% |
| | **JUMLA** | | **502,400,000** | **252,253,831** | **50%** |
| 3. | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 100,000,000 | 86,675,000 | 87% |
| | **JUMLA** | | **100,000,000** | **86,675,000** | **87%** |
| 4. | Baraza la Sanaa na Sensa na Filamu Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 148,900,000 | 111,660,418 | 75% |
| | **JUMLA** | | **148,900,000** | **111,660,418** | **75%** |
| 5. | Baraza la Taifa la Michezo | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 100,000,000 | 76,015,000 | 76% |
| | **JUMLA** | | **100,000,000** | **76,015,000** | **76%** |
| | | | | | |
| | **Jumla ya Mishahara Ruzuku** | | **214,400,000** | **163,125,015** | **76%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ruzuku** | | **802,300,000** | **461,977,483** | **58%** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,016,700,000** | **625,102,498** | **61%** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **3,088,500,000** | **2,172,958,885** | **70%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **2,602,700,000** | **1,676,693,697** | **64%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A)MATUMIZI YA KAWAIDA** | | **5,691,200,000** | **3,849,652,582** | **68%** |
| | | | | | |
| | **Miradi ya Maendeleo** | | | | |
| 1. | Maendeleo ya Vijana. | | 2,000,000,000 | - | **-** |
| 2 | Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo. | | 2,000,000,000 | 2,000,000,000 | 100% |
| | | | | | |
| | **Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)** | | 4,000,000,000 | **2,000,000,000** | **50%** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)** | | **9,691,200,000** | **5,849,652,582** | **60%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1B**
**MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2019 HADI MACHI 2020**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 230,000,000 | 113,875,900 | 49.5% |
| 2. | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 16,126,000 | 1,239,500 | 8% |
| 3. | Ofisi Kuu Pemba | 8,937,000 | 6,635,500 | 74% |
| | **JUMLA** | **255,063,000** | **121,750,900** | **48%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1C**
**MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 120,000,000 | 142,373,067 | **119%** |
| | **JUMLA** | | | |

**KIAMBATISHO NAMBA 1D**
**FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**
**Programu ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 2,308,652,000 | 196,981,680 | 8% |
| 2. | Baraza la Vijana Zanzibar | 165,400,000 | 98,498,249 | 60% |
| | **JUMLA** | **2,474,052,000** | **295,479,929** | **12%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Idara ya Utamaduni na Sanaa | 1,791,343,000 | 1,233,525,933 | 69% |
| **2** | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 148,900,000 | 111,660,418 | 75% |
| **3** | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 100,000,000 | 86,675,000 | 87% |
| 4 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 502,400,000 | 252,253,831 | 50% |
| | **JUMLA** | **2,542,643,000** | **1,684,115,182** | **66%** |

**Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 2,420,000,000 | 2,384,997,672 | 98% |
| 2. | Baraza la Taifa la Michezo | 100,000,000 | 76,015,000 | 76% |
| | **JUMLA** | **2,520,000,000** | **2,461,012,672** | **98%** |

**Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta zaVijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,438,036,000 | 915,396,727 | 64% |
| | **JUMLA** | **1,438,036,000** | **915,396,727** | **64%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 160,400,000 | 70,835,400 | 44% |
| | **JUMLA** | **160,400,000** | **70,835,400** | **44%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2019/2020 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ofisi Kuu Pemba | 556,069,000 | 422,812,672 | 76% |
| | **JUMLA** | **556,069,000** | **422,812,672** | **76%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1E**
**FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2019 HADI MACHI 2020 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 238,937,000 | 120,511,400 | 50% |
| 2. | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 16,126,000 | 1,239,500 | 8% |
| | | | | |
| 3. | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 120,000,000 | 142,373,067 | 119% |
| | **JUMLA** | **375,063,000** | **264,123,967** | **70%** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1F**
**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**
**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| IDARA | MAELEZO | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|---|
| Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 559,211,000 |
| | Matumizi Mengineo | 279,300,000 |
| **JUMLA** | | **838,511,000** |
| Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 170,000,000 |
| **JUMLA** | | **170,000,000** |
| Uendeshaji na utumishi | Mishahara | 793,725,000 |
| | Matumizi Mengineo | 680,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,473,725,000** |
| Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 148,915,000 |
| | Matumizi Mengineo | 155,000,000 |
| **JUMLA** | | **303,915,000** |
| Utamaduni na Sanaa | Mishahara | 1,355,948,000 |
| | Matumizi Mengineo | 300,000,000 |
| **JUMLA** | | **1,655,948,000** |
| Idara ya Michezo | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 630,000,000 |
| **JUMLA** | | **630,000,000** |
| **Jumla ya Mishahara** | | **2,857,800,000** |
| **Jumla ya Matumizi mengine** | | **2,214,300,000** |
| **Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **5,072,100,000** |
| **TAASISI ZA RUZUKU** | | |
| Baraza la Vijana Zanzibar | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 217,200,000 |
| **JUMLA** | | **217,200,000** |
| Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | Mishahara | 222,800,000 |
| | Matumizi Mengineo | 366,800,000 |
| **JUMLA** | | **589,600,000** |

| | | |
|---|---|---|
| Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 216,000,000 |
| **JUMLA** | | **216,000,000** |
| Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 148,400,000 |
| **JUMLA** | | **148,400,000** |
| Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - |
| | Matumizi Mengineo | 147,200,000 |
| **JUMLA** | | **147,200,000** |
| | | |
| **Jumla ya Mishahara Ruzuku** | | **222,800,000** |
| **Jumla ya matumizi mengineo ruzuku** | | **1,095,600,000** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,318,500,000** |
| | | |
| **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **3,080,600,000** |
| **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **3,309,900,000** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A** | | **6,390,500,000** |

| **Miradi ya Maendeleo** | | |
|---|---|---|
| Mradi wa Maendeleo ya Vijana | | 2,000,000,000 |
| Uimarishaji wa viwanja vya Michezo | | 2,500,000,000 |
| **Jumla ya miradi ya maendeleo B** | | **4,500,000,000** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA ( A + B)** | | **10,890 ,500,000** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1G**

**BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KWA KILA PROGRAMU NDOGO**

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1. | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 303,915,000 |
| 2. | Baraza la Vijana Zanzibar | 217,200,000 |
| 3 | Programu ya Ajira kwa Vijana | 2,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **2,521,115,000** |

**Programu Ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1. | Idara ya Utamaduni na Sanaa | 1,655,948,000 |
| 2. | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 148,400,000 |
| 3. | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 216,000,000 |
| 4. | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | 589,700,000 |
| | **JUMLA** | **2,609,948,000** |

**Programu Ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1. | Idara ya Michezo | 630,000,000 |
| 2. | Baraza la Michezo | 147,200,000 |
| 3. | Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo | 2,500,000,000 |
| | **JUMLA** | **3,277,200,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| **1.** | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 170,000,000 |
| | **JUMLA** | **170,000,000** |

**Programu Ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1. | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,473,725,000 |
| | **JUMLA** | **1,473,725,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | Ofisi Kuu Pemba | 838,511,000 |
| | **JUMLA** | **838,511,000** |

**KIAMBATISHI NAMBA 1H**
**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**
**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|---|
| 1. | Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni | 215,141,000 |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 4,000,000 |
| 3 | Ofisi Kuu Pemba | 9,000,000 |
| | **JUMLA** | **228,141,000** |

**KIAMBATISHO NAMBA 1I**
**MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2020/2021 |
|---|---|---|
| 1 | Afisi ya Msajili wa Hakimiliki | **150,000,000** |
| | **JUMLA** | **150,000,000** |

**KIAMBATISHO NAMBA 2**

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MIPINDUZI KWA KIPINDI CHA MIAKA 52015-2020

**SEKTA YA VIJANA**

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **131 A** | Kuandaa Programu za Elimu na Malezi Bora kwa Vijana ili kuwawezesha jumla ya vijana 235,817 kupata mafunzo ya stadi mbalimbali za maisha pamoja na kujiajiri; | Serikali kupitia Wizara ya Vijana Utamaduni, Sanaa na Michezo imefanikiwa kutoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana 23,895. Mafunzo yaliyotolewa ikiwemo madhara ya mimba na ndoa za umri mdogo, Elimu ya Ukimwi, Madawa ya kulevya na mimba za utotoni mafunzo haya yalitolewa Unguja na Pemba. |
| **131 B** | Kuliendeleza Baraza la Taifa la Vijana ili kuongeza ushiriki wa vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi; | Serikali imeanzisha na inayaendeleza mabaraza ya Vijana kuanzia ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa. Aidha, ushiriki wa vijana umeongezika katika ngazi mbalimbali za maamuzi ambapo idadi ya wanachama imefikia 17,540 wakiwemo (wanawake 9,137 na wanaume 8,403). Vile vile, Serikali imeweza kuwapatia Baraza la Vijana sekretarite kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa Baraza la Vijana Zanzibar pamoja na ushiriki wa Vijana. Aidha, ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya ofisi zikiwemo laptop, printa, projekta, meza na viti umefanyika kwa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya na Taifa na Serikali imewajengea uwezo viongozi wa Baraza la Vijana Zanzibar jumla ya viongozi 2,549 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali, stadi za maisha, uongozi, kilimo, uandishi wa habari, utunzaji fedha, elimu ya biashara, utalii, uibuaji wa fursa za kiuchumi na uendeshaji. Pia, Serikali imeandaa rasimu ya awali ya kanuni za uendeshaji za Baraza la Vijana Zanzibar na tovuti ya Baraza la Vijana imeanzishwa ambayo ni **www.zyc.or.tz** na wamepatiwa kanzidata. Aidha watumishi wapya watano wa Baraza la Vijana wamepatiwa mafunzo na limeandaa na kushiriki vipindi mbalimbali vya redio na televisheni za Serikali na za binafsi kwa lengo la kutoa elimu kwa Vijana kuhusiana na Mabaraza ya Vijana na faida zake. |
| **131 C** | Kuendelea kuimarisha Mfuko Maalumu wa Vijana ili kutoa mikopo kwa vijana wengi zaidi na kujiajiri katika kilimo cha kisasa na kuanzisha *"Green House"* moja katika kila wilaya; | Serikali imeunganisha Mfuko wa Vijana na Mfuko wa Uwezeshaji na imeendelea kuwahamasisha na kuwaunganisha vijana na huduma za mikopo kupitia mfuko wa uwezeshaji. Pia, Serikali imetoa mafunzo kwa Vijana 40 yanayohusu kilimo na ufugaji Pemba, mafunzo hayo yalihusisha namna ya kutafuta masoko, usindikaji wa mazao na utengenezaji wa mbolea. Vile vile, imefanya utafiti juu ya kilimo cha hema kujua kinawekezana kutekelezeka kwa ajili ya kuwawezesha vijana. Utafiti huo umebaini kuwa kilimo hicho kinawezekana kutumika na kukuza na kutoa tija kwa wakulima wataokitumia na kwa Taifa. Utafiti huo umebaini pia, kuwepo kwa "Green house" 16 kwa upande wa Unguja na "Green house" 2 kwa upande wa Pemba zinazoendeshwa na kusimamiwa na vijana. Pamoja na hayo, Serikali |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| | | imewapatia elimu Vijana ya kutumia fursa ya ujuzi wa kilimo cha kisasa kupitia Program ya kilimo endelevu "Fursa Kijani ". Aidha, utafiti mdogo umefanyika wa kuvigundua vikundi vya vijana vinavyojishughulisha na shughuli za kiuchumi na kujua mahitaji yao Unguja na Pemba. Katika utafiti huo jumla ya vikundi 87 kwa Wilaya zote vilitembelewa. Aidha Wizara kupitia programu ya Ajira kwa Vijana inaendelea na ujenzi wa "Green House" 19 kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Jumla ya vijana 890 watanufaika na kilimo hicho katiaka hao 480 Unguja na 410 Pemba. Aidha, jumla ya vijana 350 wamewezeshwa katika maeneo ya ufugaji wa kuku, nyuki na samaki, aidha kwa upande wa mradi wa pili pili jumla ya vijana 320 wanatarajiwa kunufaika. |
| **131 E** | Kuandaa mikakati ya malezi bora kwa vijana ili kujenga moyo wa uzalendo, ari ya kujitolea na kuipenda nchi yao na kuimarisha mahusiano ya vijana ndani na nje ya nchi. | Serikali inaendelea kushajiisha vijana kushiriki katika shughuli mbali mbali za Kitaifa na Kimataifa katika kuwajengea moyo wa uzalendo kwa kushiriki katika matukio mbali mbali yakiwemo Mbio za Mwenge wa Uhuru, Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Siku ya Mashujaa na maadhimisho ya siku ya Kimataifa ya vijana Duniani. Makongamano matano na bonanza moja yaliandaliwa kwa ajili ya kuamsha ari ya uzalendo kwa vijana. |
| **172 (a)** | Kuendelea kuwashirikisha vijana kwa kuwapa nafasi za maamuzi katika ngazi zote kutegemeana na sifa, uweledi na uadilifu. | Serikali imewajengea uwezo vijana kupitia Mikutano mbali mbali ya Mabaraza ya Vijana ikiwemo Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana Taifa na Mikutano ya Baraza la Watendaji pamoja na Mikutano yao mikuu inayofanyika katika kila Wilaya na Shehia. |
| **172 (b)** | Kuwaandaa na kuwawezesha Vijana kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za Baraza la Taifa la Vijana. | Serikali imewawezesha Vijana kushiriki katika matukio mbali mbali yanayohusu Baraza la Vijana la Taifa ikiwemo Mkutano Mkuu wa Baraza la Vijana Zanzibar na Mkutano wa Baraza la Watendaji Taifa na ikijumuisha mikutano yote inayofanyika katika Mabaraza ya Vijana Wilayani na Shehia. Vile vile, Serikali imesimamia ushiriki wa vijana kwenye mikutano mbalimbali inayowahusu ikiwemo, Mikutano ya kikanda, Midahalo, Makongamano pamoja na mafunzo mbalimbali ambapo zaidi ya Vijana 293 wameshiriki katika shughuli hizo. |
| **172 C** | Kuendelea kutoa elimu kwa vijana kwa kuwatumia wahusika mbali mbali ili kuwajenga kuwa wazalendo na kuepuka vishawishi vitakavyowaharibia malengo yao ya baadaye. | Serikali imewasiliana na washirika wa maendeleo wanaoshughulikia vijana na kuwaunganisha vijana na fursa za Ujuzi wa kupata ajira na uzalishaji ikiwa ni pamoja na UNFPA, PPIZ, Milele Zanzibar Foundation, VSO na Eqwip Hubs. Jumla ya Vijana 60 (30 kutoka Pemba na 30 Unguja) waliunganishwa na fursa mbali mbali ikiwemo kilimo na ujasiriamali. Aidha, imewajengea uelewa vijana 140 kutoka mabaraza ya vijana na taasisi za vijana juu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana na Mkataba wa Maendeleo ya Vijana Afrika kujua mikakati ya utekelezaji wa miongozo hiyo ili kuweza kuzingatia katika shughuli zao. Pia, Serikali inaendelea na hatua |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| | | mbali mbali za ushajihishaji wa vijana kujiunga na Program ya U report (Jukwaa la Vijana kutoa maoni kupitia Mtandao) katika wiki ya vijana na kumbukumbu ya Baba wa Taifa. Vijana 1,120 (Wanaume 598 na Wanawake 522) walifikiwa Unguja na Pemba. Aidha, Vijana 1,300 walijiunga na jukwaa la U report na vijana 25500 walipatiwa mafunzo kuhusiana na U-report. Vile vile, Vijana wa kike 1,565 walipatiwa mafunzo ya uzalendo pamoja na kuhamasishwa katika kushiriki nafasi mbali mbali za uongozi. |
| **172 E** | Kuanzisha uraghibishi kwa vijana waweze kujiajiri kwa kuthamini kazi nyingine za mikono na utalamu kama vile kilimo, ufundi, michezo, sanaa na kazi nyingine za kitaaluma. | Serikali imetembelea na kufanya ufuatiliaji katika taasisi mbali mbali za vijana ili kujua shughuli zao za maendeleo wanazozifanya na changamoto zinazowakabili. Miongoni mwa tasisi zilizotembelewa ni pamoja na ZAYDO, SCOUTI, TAYI, MYDO, EQWIP HUBS, MILELE ZANZIBAR FOUNDATION, PPIZ. Pia imetembelea vikundi 60 vya ujasiriamali vya vijana ambao waliopatiwa mikopo na saccos ya vijana ili kuangalia maendeleo yao na imefanya ufuatiliaji wa vikundi vya kiuchumi vya vijana na jumla ya vikundi 95 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba vilifuatiliwa na kubaini shughuli zao za kiuchumi, mafanikio na changamoto zinazowakabili na kupewa ushauri. |

**SEKTA YA UTAMADUNI NA SANAA**

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **113 B** | Kuimarisha lugha ya Kiswahili na kuzifanya lahaja za Kiswahili za Zanzibar kuwa chimbuko la Kiswahili fasaha. Jumla ya machapisho mapya 10 ya vitabu na majarida 15 ya kuimarisha lugha ya Kiswahili yatatolewa kwa lengo la kuwawezesha watumiaji wenyeji na wageni kukitumia Kiswahili fasaha katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii; | Vipindi 214 kupitia TV na Redio za Serikali na binafsi vimerushwa kwa lengo la kutoa taaluma juu ya matumizi sahihi na fasaha ya lugha ya Kiswahili na makongamano mbalimbali ya Kimataifa yalilowashirikisha wageni mbali mbali kutoka nje ya nchi yalifanyika kwa lengo kukiendeleza Kiswahili. Aidha, imefanikiwa kutoa makamusi 13,334 ya Lugha ya Kiswahili katika Taasisi zote za Serikali, skuli zote za Serikali na binafsi za Unguja na Pemba kwa lengo la kusaidia jamii kutumia Kiswahili kwa ufasaha na usanifu. Pia machapisho mawili na nakala zake zimesambazwa. Serikali inaendelea na uandaaji wa Sera ya lugha ya Kiswahili, ili kudhibiti matumizi mabaya ya lugha. Kamusi la viumbe vya baharini limehaririwa kwa kunyoosha, kuweka sawa na kuviwekea fasili vidahizo ambavyo vilikuwa havina fasili pamoja na kuhakiki visawe vilivyomo. Pamoja na hayo miswada mitano ikiwemo mswada wa kamusi la Kiingereza na Kiswahili, mswada wa kitabu cha Mawasiliano ya Msingi ya Kiswahili kwa wageni cha Kiswahili Kifaransa, mswada wa kitabu cha Utamaduni wa Mzanzibari kwa Lugha ya Kiingereza, mswada wa kitabu cha Hadithi fupi na mswada wa Jarida namba 4 la Jahazi imetayarishwa. Vile vile Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyenige za lugha imefanikisha kushwawishi lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya nnne itakayotumika katika vikao vya nchi wanachama wa SADC |
| **113 C** | Kuihamasisha jamii ili kuuenzi, kuulinda na kuudumisha utamaduni wa Mzanzibari na kushiriki katika uandaaji wa matamasha 50 ya utamaduni; | Serikali imefanikiwa kuadhimisha Tamasha la 24 La Utamaduni wa Mzanzibari na maadhimisho ya tamasha hilo lilifanyika Unguja na Pemba. Vikundi mbalimbali vya ngoma za kiasili, Vikundi vya wajasiriamali wa kazi na bidhaa za kiutamaduni, vyakula vya kiasili, taraabu asilia, Maulidi ya homu, usiku wa sanaa, michezo na nyimbo za watoto, mchezo wa ng'ombe, muziki wa kizazi kipya, makongamano kuhusu nafasi na fursa za kiutamaduni kwa vijana yalifanyika. Aidha, Serikali imeratibu na kushiriki katika maandalizi ya matamasha 29 ya Utamaduni yakiwemo Tamasha la vyakula vya asili ya kimakunduchi, Tamasha la Utamaduni la Rafiki network, Tamasha la Elimu bila ya malipo, Tamasha la Nchi za Jahazi (ZIFF), Tamasha la Watu wa Mangapwani, Tamasha la Muziki wa |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| | | JAZZ, Tamasha la Mwaka kongwa na tamasha la urithi wa Mtanzania. |
| **113 D** | Kuwapatia mafunzo walimu 150 wa utamaduni na wasanii 500 ili kuwawezesha kutumia sanaa zao kwa mambo yenye manufaa kwa wananchi na yenye kuzingatia maadili ya jamii; na | Serikali imewapatia mafunzo ya utamaduni walimu 543 wa somo la utamaduni, maofisa Utamaduni wa Wilaya 11 na wanafunzi 87 wa skuli za msingi Unguja na Pemba. Pia, wasanii 752 wa filamu na maigizo wamepatiwa mafunzo ya sanaa na mbinu za uwandishi ya maswali ya Filamu, uandishi wa miswada ya filamu, ubunifu wa wahusika, mandhari, haki na mikataba katika uzalishaji wa kazi za sanaa, kutambuwa fursa za kiutamaduni na zile za Mashirika ya kifedha na kuzitumia.<br>Vile vile, wasanii 33 walipatiwa mafunzo katika fani ya uchoraji, ushonaji na uchapishaji, na urithi juu ya tamaduni zetu. |
| **113 E** | Kuendeleza teknolojia za jadi kwa kutoa mafunzo kwa mafundi 75 ili yaweze kuwanufaisha wananchi kiuchumi na kurithisha teknolojia hiyo kwa kizazi kipya. | Serikali imekamilisha utafiti wa kuwatambua mafundi na sasa imo katika hatua ya uchambuzi wa taarifa za mafundi hao na aina ya vifaa na teknolojia za jadi wanazozitumia, ambapo zitawanufaisha wananchi kiuchumi na kurithisha teknolojia hiyo kwa vizazi vijavyo. |
| **159 A** | Kuhakikisha lugha ya Kiswahili inaendelezwa ndani na nje ya nchi na kutumika kama bidhaa ya soko na chanzo cha ajira kwa wataalamu na wapenzi wa Kiswahili. Aidha, kupanua wigo wa misamiati na istilahi za lugha za Kiswahili kwa kufanya utafiti wa Lugha za Kijamii; | Baraza la Kiswahili limeshiriki Makongamano ya Kiswahili yalioandaliwa na vyama mbalimbali ikiwemo chama cha lugha na fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), ambapo mada zilizojadiliwa zililenga Vijana, Lugha na Uchumi wa viwanda na chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) Zanzibar. Wizara imefanikiwa kuandaa kongamano la Tatu la Kiswahili la Kimataifa lililoshirikisha washiriki 656 kutoka nchi mbambali kama vile Tanzania, Marekani, Misri, Sweeden, Rwanda, Austria, Uganda, Pakistan, Kenya, Burundi na Zanzibar.<br>Vile vile, Wizara kwa kupitia Baraza la Kiswahili imetoa mafunzo kwa waandishi chipukizi wa hadithi fupi na kufanya mashindano ya hadithi fupifupi kwa wanafunzi wa Sekondari na Vyuo Vikuu. |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **159 C** | Kusimamia Utekelezaji wa Sheria zinazohusu shughuli za Filamu, Michezo ya Kuigiza, Muziki, Ubunifu kwa lengo la kulinda haki na Maslahi ya Makundi hayo; na | Katika kuhakikisha maslahi ya wasanii yanaimarika. Jumla ya Shilingi 166,680,921 za mirabaha zimekusanywa na kugaiwa kwa wasanii na wabunifu 2,514. Aidha, wabunifu na wasanii 79 wagonjwa wamefikiwa katika maeneo yao na kuwapatia kiasi cha fedha kinachotokana na sehemu maalum ya mirabaha. Kanuni 3 za Usimamizi wa hakimiliki zimeandaliwa. Aidha, Serikali imefanya mazingatio pamoja na mfumo uliopo wa kawaida wa mahkama, yakuanzisha mfumo wa usuluhishi (Copyright Dispute Settlement). |
| **163(a)** | Kuendeleza kuimarisha uwezo wa bodi ya filamu nchini ili isimamie kwa ukamilifu maendeleo ya tathnia ya filamu kwa kuendeleza ujuzi wa sekta hii. | Serikali imekutanisha bodi ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni kujadiliana maendeleo ya Sanaa na wasaniii pamoja na kuwaongoza wasanii kufanya kazi zao kulingana na Utamaduni na mila zetu. |
| **163 D** | Kuendeleza programu za Ujasiriamali kwa vijana na makundi mbalimbali kwa kutoa ushauri, mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi kwa wajasiriamali walio katika tasnia ya sanaa na kuweka msukumo mkubwa katika maendeleo ya tasnia ya sanaa; | Vijana 62 wameendelezwa kwa kupatiwa mafunzo na huduma za kiufundi za ujasiriamali katika tasnia ya Sanaa ili waweze kujiajiri wenyewe. Aidha, Vijana 44 wameendelezwa kwa kupatiwa mafunzo na huduma za kiufundi kama nyenzo ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe. Vile vile, vijana 150 wamepatiwa taaluma na ushauri juu ya matumizi ya fursa zinazopatikana kupitia sanaa na utamaduni Unguja na Pemba. Aidha jumla ya vikundi 36 vya wajasiriamali na vikundi 6 vya sanaa za maonesho vilishiriki katika maadhimisho ya Tamasha la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) Dar-Es-Salaam Tanzania na kupatiwa huduma za kiufundi juu ya namna bora ya kushiriki katika matamasha ya kimataifa. |
| **163 F** | Kuhakikisha kazi za wasanii zinalindwa ili zisighushiwe wala kuibiwa. | Serikali imefanya ukaguzi wa Maduka yote ya vinasa sauti ili kuzuwia uharamia wa kazi za wasanii ambapo jumla ya watumiaji 256 wa kazi za Hakimiliki kibiashara wamekaguliwa wakiwemo wenye maduka ya kuuza na kukodisha kazi za vinasa sauti vya kusikia na kuona (180), Mahoteli (75) Kumbi za Burudani (1). Aidha Watumiaji hao walielimishwa juu ya matumizi sahihi ya kazi za hakimiliki, kuepuka uharamia na umuhimu wa kulipia mirabaha ili waweze kufanya biashara zao kihalali. |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **163 G** | Kuhakikisha wasanii wanapata maslahi wanayostahili kutokana na kazi zao kwa kuboresha mazingira ya kisheria. | Katika kuhakikisha maslahi ya wasanii yanaimarika. Jumla ya Shilingi 262,501,333 za mirabaha zimekusanywa kutoka kwa watumiaji mbalimbali na na zitagaiwa kwa wasanii na wabunifu 1,280 wa vikundi mbalimbali vya sanaa na ubunifu vikiwemo vikundi vyaTaarab, Muziki wa kizazi kipya, Muziki wa Injili, Kasida, filamu na Maigizo. Aidha Wabunifu na wasanii 75 wagonjwa wamefikiwa katika maeneo yao na kuwapatia kiasi cha fedha kinachotokana na sehemu maalum ya mirabaha. Vile vile, Kanuni ya usimamizi wa kazi za maandishi imeanza kufanya kazi (The Copyright Procedures for Rent or Reproduction of Copyright Works Regulations) na Afisi imefanya upembuzi wa kuelewa kiwango cha utumiaji wa kazi za maandishi kibiashara katika taasisi za elimu na maeneo ya watumiaji. Aidha mirabaha ya kazi hizo imeanza kukusanywa |
| **163H** | Kuweka msukumo katika kuhakikisha kwamba shughuli na biashara za Sanaa ikiwemo filamu, ngoma za asili, michezo ya kuigiza nyengine za ubunifu zimerasishwa ili kuendeleza tasnia hii na wasanii wenyewe. | Serikali kupitia Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni imeweza kurasimisha jumla ya kazi za Sanaa 11 kwa lengo la kuendeleza tasnia na wasanii wenyewe. Aidha, filamu 500 za kazi za Sanaa, maduka ya filamu 142 na maonesho 89 yajukwaani yamekaguliwa na kuhakikiwa ili kuweza kwenda sambamba na maadili, mila na silka za Kizanzibari na kuingia katika soko la ndani na nje kwa manufaa ya nchi na wanachi. |
| **163 I** | Kuanzisha maeneo changamani ya shughuli za utamaduni nchini kwa kujenga miundombinu ya kisasa; | Serikali imekamilisha ujenzi wa studio ya kurikodia Filamu iliyopo Rahaleo, Muziki na Michezo ya kuigiza kwa kunyanyua vipaji na uwezo wa wasanii na kuzalisha kazi zenye ubora. |
| **163 K** | Kuhifadhi kumbukumbu ya ushiriki na mchoro wa Tanzania katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika kwa kuendeleza utekelezaji wa Programu ya Urithi wa ukombozi | Serikali imepeleka Dodoma wajumbe katika Kamati ya Kitaifa ya wataalamu wa programu ya urithi wa ukombozi wa Bara, Kamati hiyo imefanikiwa kuyaainisha na kuayatambua maeneo yalioshiriki katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika kwa kuendeleza utekelezaji wa Programu hiyo Pamoja na kuufanyia marekebisho mpango wa utekelezaji wa programu hiyo |

**SEKTA YA MICHEZO**

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **111 A** | Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo kwa lengo la kuimarisha afya zao na kuendeleza Michezo ya Asili hususan mchezo wa Ng'ombe na mashindano ya resi za ngalawa na kutumia sanaa za aina mbalimbali ili kujiajiri wao wenyewe kwa lengo la kupambana na umasikini; | Katika kuwahamasisha wananchi kushiriki michezo ili kulinda afya zao, Serikali iliweka utaratibu ifikapo tarehe 1, Januari ya kila mwaka kuwa ni siku ya mazoezi kitaifa kwa vikundi tofauti vya mazoezi na kuwashirikisha watu wote Unguja na Pemba. Vikundi vya mazoezi ya viungo vilivosajiliwa vimeongezeka kutoka 36 mwaka 2016 hadi kufikia vikundi 81 mwaka 2019 ambapo kwa Unguja ni 43, Pemba 27 na Tanzania Bara 11. Kwa upande wa michezo ya Asili Serikali imeendela kukuza na kuimarisha michezo hiyo ambapo mchezo wa ng'ombe umeendelea kukuzwa, kuendelezwa na kuimarishwa ukiwa ni sehemu ya urithi wa utamaduni. Pia resi za ngalawa, mchezo wa bao na karata huchezwa kila mwaka katika maadhimisho ya wiki ya tamasha la utamaduni la Mzanzibar na katika sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. |
| **111 B** | Kukiimarisha Kituo cha Michezo cha Dole ***(Dole Academy)*** ili kuendeleza michezo ya aina mbalimbali kwa vijana na kuanzisha mfumo wa michezo ya kulipwa na kushiriki mashindano ya Kimataifa; | Serikali inaendelea na hatua za kukiimarisha kituo cha michezo cha 'Dole Academy' ili kuendeleza michezo ya aina mbali mbali kwa vijana pamoja na kuanzisha mfumo wa michezo ya kulipwa na kushiriki mashindano ya Kimataifa. Katika muendelezo wa hatua hizo, Serikali imefanya tathmini ya awali ya kukiendeleza kituo hicho kwa lengo la kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanamichezo nchini.<br>Serikali imeziwezesha timu zetu kushiriki mashindano ya kimataifa ili kuonyesha vipaji vyao na kimataifa na hatimae kupata nafasi za kujiunga na timu za nje. Timu zilizowezeshwa kushiriki mashindano ya kimataifa ni kama zifuatazo: - Zanzibar Heroes, KMKM, Mafunzo, JKU, Timu ya Riadha ya Zanzibar, Timu ya soka la ufukweni (Beach Soccer), Jamhuri, Jang'ombe Boys, KVZ, KZU, Taifa ya Jang'ombe, Timu ya mpira wa pete, wanyanyua vyuma vizito. Timu hizo zilishiriki katika mashindano ya Challenge CUP, Klabu bingwa Barani Afrika, Kombe la Mapinduzi, Afro Asia Weightlifting Championship na CECAFA nchini Uganda. |
| **111 C** | Kujenga viwanja vya michezo katika Wilaya tano (5) na kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa vijana ili kuwaongezea ujuzi na uzoefu wa michezo kwa kutumia walimu wa ndani na nje ya nchi; | Serikali imekamilisha ujenzi wa viwanja 3 vya Michezo vya Wilaya ambavyo ni Kiwanja cha Kitogani Wilaya ya Kusini- Unguja, kiwanja cha Kishindeni Wilaya ya Micheweni na Kangani Wilaya ya Mkoani Pemba. Ujenzi wa viwanja umesaidia katika kupunguza tatizo la viko katika hatua ya mwisho. Pia, uhaba wa viwanja. Aidha Wizara inaendelea na taratibu za ujenzi wa viwanja 2 vilivyobakia ambayo ni Mkokotoni Wilaya ya Kasakazini "A" na Kama Wilaya ya Magharibi "A". Pia imesaidia vifaa vya michezo kwa vyama saba, Chama cha Mchezo wa Riadha na Chama cha Mchezo wa Mpira wa Wavu, chama cha Mpira wa Miguu, chama cha Mpira wa kikapu, Chama cha Viziwi, Chama cha Karata naa Chama cha Bao. Vile vile, imewapatia mafunzo Makocha na Waamuzi 102 Unguja na Pemba ambapo 56 |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| | | kutoka Unguja na 46 kutoka Pemba. Vile vile, jumla ya makocho 35 wamepatiwa mafunzo ya kati (Intermediate level) wa chama cha Riadha kutoka Unguja na Pemba. |
| **111 D** | Kukifanyia matengennezo makubwa kiwanja cha michezo cha "Mao - Zedong" ili kiweze kutumika kwa shughuli za michezo na sherehe za kitaifa; na | Serikali imefanikiwa kukifanyia matengenezo makubwa kiwanja cha michezo cha Mao -Zedong kushirikiana na Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China kwa unjenzi wa viwanja viwili vya mpira sambamba na uwekaji wa nyasi bandia, ujenzi wa kiwanja mchanganyiko na kiwanja cha michezo ya ndani(indoors game), kiwanja cha mazoezi ya viungo (gym), ujenzi wa vyoo 48, majukwaa ya wageni mashuhuri na watizamaji wa kawaida, ujenzi wa ofisi mbili, ujenzi wa sehemu za pembembezoni mwa uwanja (edges) pamoja na ujenzi wa ukuta. |
| **111 E** | Kuvipatia vyama vya michezo vya watu wenye ulemavu fursa stahiki ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuendeleza michezo ikiwemo ya kulipwa. | Serikali imewawezesha viongozi wa Shirikisho la Mchezo wa Viziwi kushiriki mafunzo ya uongozi ya Kimataifa Johanasbarg Afrika Kusini August 2018, imekiwezesha chama hicho kuhamasisha michezo ya Viziwi Unguja na Pemba, Novemba, 2018 na imewawezesha Kiongozi na mchezaji wa michezo ya Watu Wenye Ulemavu wa akili kuungana na Timu Taifa ya Tanzania kushiriki mashindano ya Dunia yaliyofanyika nchini Abudhabi, Machi, 2019. Aidha, chama hicho kimesaidiwa kushiriki katika mkutano wa viongozi uliofanyika Oktoba 2018, Dar es Salaam.<br>Vile vile, timu ya Taifa ya Mchezo ya Watu wenye Ulemavu wa Viungo imeshiriki mashindano ya Kimataifa ya mchezo huo yaliyofanyika Dar es Salaam June, 2019. Pamoja na hayo Shirikisho la Michezo ya Viziwi liliwezeshwa kushirikia katika michezo ya Viziwi yaliyofanyika nchini Uganda, Mwezi Agosti, 2019. Aidha, jumla ya wanamichezo 9 kupitia vyama vya watu wenye mahitaji maalum wamepatiwa fursa ya kushiriki mafunzo ya utawala na uongozi pamoja na mafunzo ya Riadha ngazi ya kati yaliyofanyika mwezi wa Febuary 2020. |
| **161 A** | Kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo nchini; | Serikali imeweza kuufanyia matengenezo Uwanja wa Amani katika jukwaa la Watu mashuhuri (VIP) na kujaza udongo katika viwanja vya nje vya uwanja wa Amaan, kuweka palate kwenye mageti ya Uwanja huo na kujenga uzio wa matofali katika kiwanja hicho. Pia, upakaji rangi Uwanja wa Gombani umefanyika. Uwekaji tatan katika Uwanja wa Gombani Pemba. |

| Ibara | Maagizo ya Ilani | Utekelezaji hadi 2019 |
|---|---|---|
| **161 C** | Kuhamasisha na kusisimua Maendeleo ya Michezo katika ngazi zote hapa nchini kwa kuendeleza matamasha ya Michezo kuanzia ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa; | Serikali imeweza kuandaa Tamasha la kitaifa la siku ya mazoezi ya Viungo ambalo hufanyika kila mwaka ifikapo tarehe 1 Januari kwa mwaka 2018 limefanyika katika uwanja wa Amaan Unguja na kwa mwaka 2019 limefanyika katika Uwanja wa Gombani Pemba Mgeni Rasmi alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein. Vile vile, Serikali kupitia Baraza la Michezo Taifa imefanya Bonanza dogo la Mazoezi ya viungo Disemba, 2018.<br>Aidha, Wizara imeweza kuhamasisha uanzishaji wa matamasha na michezo mbali mbali nchini ikiwemo michezo maarufuwa ya Yamle yamle cup ambayo hushirikisha timu kutoka Wilayani, Mapinduzi Toto cup ambayo husaidia kuibua vipaji vya vijana kuanzia ngazi ya Shehia, Wilaya hadi Mkoa. Vile vile, Kadhalika Idara Wizara imefanikiwa kuandaa na kusimamia mashindano ya mawizara, taasisi na mashirika ya uma ambayo yameleta hamasa kubwa kwa watumishi na watendaji wa serikali. |
| **161 E** | Kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo na burudani kwa kushirikiana na makundi ya wanamichezo, jamii na mamlaka nyengine. | Serikali imesimamia kupatikana kwa hatimiliki za viwanja vya Tibirinzi, Nungwi na Gombani. |
| **161 G** | Kuendelea kufundisha wataalamu wa michezo na kuhakikisha wanapatikana katika ngazi zote | Serikali imefanikiwa kuwapatia fursa za mafunzo Makocha wa Michezo wa Riadha, mchezo wa Taekondo ITF, SOS na ZAD na mafunzo ya utawala na uongozi ili kuengeza ufanisi katika Michezo. Hadi kufikia 2020 idadi ya Waamuzi na viongozi 72 kwa vyama vya michezo wamepatiwa fursa ya kushiriki na kupata mafunzo ndani na nje ya nchi. |

**KIAMBATANISHO NAMBA 3A**

VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOFAIDIKA NA PEMBEJEO ZA KILIMO UNGUJA NA PEMBA

| WILAYA | KIKUNDI | JUMLA YA VIJANA |
|---|---|---|
| KASKAZINI "A" | CHAANI KIKOBWENI | 36 |
| | NA SISI TUPO DONGE MCHANGANI | 20 |
| | BARAZA LA VIJANA TUSHIKAMANE | 9 |
| | **JUMLA** | **65** |
| KASKAZINI "B" | MAKOBA | 28 |
| | MAFUFUNI | 40 |
| | MISUFINI | 22 |
| | **JUMLA** | **90** |
| KUSINI UNGUJA | BARAZA LA VIJANA BWEJUU | 7 |
| | BARAZA LA VIJANA NGANANI | 21 |
| | SISI KWA SISI | 20 |
| | **JUMLA** | **48** |
| KATI | HAPA KAZI TU | 30 |
| | BARAZA LA VIJANA PAGALI | 6 |
| | BARAZA LA VIJANA DUNGA BWENI | 25 |
| | **JUMLA** | **61** |
| MAGHARIBI B | DIMANI SAFI | 17 |
| | WAKOMBOZI COOERATIVE | 18 |
| | FUONI KIBONDENI | 40 |
| | **JUMLA** | **75** |
| **JUMLA KWA UNGUJA** | **VIKUNDI 16** | **339** |
| | | |
| CHAKE CHAKE | CHAKE YOUTH FARMER'S | 18 |
| | RIZIKI HAINA MJA | 30 |
| | **JUMLA** | **48** |
| MKOANI | MAKOMBENI | 55 |
| | **JUMLA** | **55** |
| WETE | KUJIKOMBOA COOPERATIVE | 25 |
| | MAISHA NI KUTAFUTA | 5 |
| | **JUMLA** | **30** |
| MICHEWENI | CHAMBONI GROUP | 22 |
| | UMOJA NI NGUVU | 13 |
| | **JUMLA** | **35** |
| **JUMLA KWA PEMBA** | **VIKUNDI 7** | **168** |
| **JUMLA KWA UNGUJA NA PEMBA** | **VIKUNDI 23** | **507** |

**KIAMBATANISHO NAMBA 3B**

VIKUNDI VYA VIJANA VITAKAVYOFAIDIKA NA VIFAA VYA USHONI UNGUJA NA PEMBA

| WILAYA | KIKUNDI | JUMLA YA VIJANA |
|---|---|---|
| KASKAZINI "A" | BARAZA LA VIJANA MUANGE | 10 |
| | HAMASA | 28 |
| | JUMLA | 38 |
| KASKAZINI B | BARAZA LA VIJANA FUJONI | 25 |
| | BARAZA LA VIJANA MANGAPWANI | 5 |
| | JUMLA | 30 |
| KUSINI | BARAZA LA VIJANA KAJENGWA | 10 |
| | TUJIKOMBOE MUUNGONI | 5 |
| | JUMLA | 15 |
| KATI | MPAPA YOUTH GROUP | 16 |
| | VIJANA IMARA | 25 |
| | JUMLA | 41 |
| MAGHARIBI A | MY AFRICAN PRODUCT KIHINANI | 8 |
| | BARAZA LA VIJANA CHUINI | 3 |
| | JUMLA | 11 |
| MAGHARIBI B | WAKOMBOZI COOPERATIVE KISAUNI | 11 |
| | | |
| MJINI | BARAZA LA VIJANA MUEMBE MAKUMBI | 15 |
| JUMLA UNGUJA | VIKUNDI 12 | 161 |
| | | |
| CHAKE CHAKE | BARAZA LA VIJANA CHAKE CHAKE | 10 |
| | VIJANA NA MAENDELEO CHANJAANI | 12 |
| | TUJIKOMBOE MGOGONI | 12 |
| | JUMLA | 34 |
| MKOANI | BARAZA LA VIJANA MWAMBE | 35 |
| | BARAZA LA VIJANA MKWACHE | 15 |
| | JUMLA | 50 |
| WETE | IMANI GROUP UTAANI | 25 |
| | BARAZA LA VIJANA JOJO | 12 |
| | JUMLA | 37 |
| MICHEWENI | UMOJA NI NGUVU MAJENZI | 8 |
| | UMOJA NI MSHIKAMANO | 40 |
| | JUMLA | 48 |
| JUMLA PEMBA | VIKUNDI 9 | **169** |
| JUMLA UNGUJA NA PEMBA | VIKUNDI 21 | **330** |

**KIAMBATANISHO NAMBA 3C**

**MCHANGANUO WA VITALU NYUMBA PAMOJA NA VISIMA NA MIUNDOMBINU YA MAJI UNGUJA NA PEMBA**

| WILAYA | KIKUNDI | KITALU NYUMBA | KISIMA NA MNARA | JUMLA YA VIJANA |
|---|---|---|---|---|
| **KASKAZINI "A"** | DONGE MCHANGANI | 1 | 1 | 130 |
| | BARAZA LA VIJANA KIKOBWENI | | 1 | 9 |
| | NASISI TUPO MCHANGANI | | 1 | 20 |
| | JUMLA | 1 | 3 | 159 |
| **KASKAZINI "B"** | PANGATUPU | 2 | 1 | 70 |
| | PANGENI | 2 | 1 | 26 |
| | BARAZA LA VIJANA KITOPE | | 1 | 30 |
| | JUMLA | 4 | 3 | 126 |
| **KATI** | KOANI | 1 | 2 | 55 |
| | JUMLA | 1 | 2 | 55 |
| **KUSINI** | KITOGANI PANGE JUU | 1 | 1 | 28 |
| | MAKUNDUCHI CHIABONDE | 1 | 1 | 130 |
| | MUUNGONI | | 1 | 24 |
| | JUMLA | 2 | 3 | 154 |
| **MAGHARIBI "B"** | KIKUNDI CHA VIJANA KIBONDENI | 1 | 1 | 40 |
| | DIMANI SAFI | | 1 | 17 |
| **MAGHARIBI A** | DOLE | 1 | 1 | 30 |
| | JUMLA | 2 | 3 | 87 |
| **JUMLA UNGUJA** | | **10** | **14** | **581** |

| WILAYA | KIKUNDI | KITALU NYUMBA | KISIMA NA MNARA | JUMLA YA VIJANA |
|---|---|---|---|---|
| **MKOANI** | MBAYAYANI YOUTH GROUP | 2 | 1 | 28 |
| | JAMBO GROUP | 1 | 1 | 25 |
| | GREEN VILLAGE | | 1 | 16 |
| | UTANDAWAZI COOPERATIVE SOCIETY | | 1 | 32 |
| | HATUKATI TAMAA NGWACHANI TANGAANI | | 1 | 14 |
| | GREEN VILLAGE KANGANI | | 1 | 16 |
| | KITANDU MGAGADU | | 1 | 22 |
| | JUMLA | 3 | 7 | 153 |
| **CHAKE CHAKE** | CHONGA KIPAPO | | 1 | 22 |
| | RIZIKI HAZINA MJA KIBOKONI | | 1 | 30 |
| | RIZIKI HAINA MJA MJINI OLE | 2 | 1 | 26 |
| | KIBOKONI | | 1 | 30 |
| | UWANDANI | | 1 | 25 |
| | JUMLA | 2 | 5 | 133 |
| **WETE** | CHAMANANGWE | 1 | 1 | 27 |
| | KUJIKOMBOA COOPERATIVE GANDO | | 1 | 25 |
| | NIA YETU MGOGONI | 1 | 1 | 20 |
| | MGOGONI | | 1 | |
| | JUMLA | 2 | 4 | 72 |
| **MICHEWENI** | TUMBE | 1 | 1 | 27 |
| | SHUMBA VIAMBONI | 1 | 1 | 25 |
| | JUMLA | 2 | 2 | 52 |
| **JUMLA PEMBA** | | **9** | **18** | **410** |
| **JUMLA UNGUJA NA PEMBA** | | **19** | **32** | **923** |

**KIAMBATANISHO NAMBA 3D**

**VIKUNDI VYA WATU WENYE ULEMAVU VILIVYOFAIDIKA NA VIFAA UNGUJA NA PEMBA**

| WILAYA | KIKUNDI | JUMLA YA WALIOFAIDIKA |
|---|---|---|
| KASK AZINI "A" | KIBENI MILLING COOPERATION | 14 |
| | TUFIKIRIENI TJONGOE | 42 |
| | MASIKINI NAO WATU | 31 |
| | TUMUAMINI MUNGU | 29 |
| | JUMLA | 116 |
| KASKAZINI "B" | UMOJA NI UTU BUMWINI MISUFINI | 17 |
| | JUMLA | |
| KUSINI | CHUMA UTUMIE MTENDE | 17 |
| | UFUGAJI WA KUKU MUYUNI C | 9 |
| | JUMLA | **36** |
| KATI | NA SISI TUWE MBELE MPAPA | 19 |
| | HAKUEKI UROA | 27 |
| | MOLA TUPE NDIJANI MSEWENI | 10 |
| | UJUAO WAKATI CHWAKA | 13 |
| | NA SISI NI WAJA MGENI HAJI | 15 |
| | NA SISI TUHURUMIENI TUNDUNI | 20 |
| | HATUBAGUANI JENDELE | 13 |
| | POA MOYO MPAPA | 37 |
| | SIRI YETU TUNGUU | 31 |
| | FALYATANADHAF TUNGUU | 4 |
| | NASISI WAJA BAMBI | 15 |
| | JUMLA | 204 |
| MAGHARIBI A | DIS ABILTY VEGETABLE | 11 |
| MAGHARIBI B | NA SISI NI WAJA KINUNI | 21 |
| | UPENDO CENTRE MWANAKWEREKWE | 48 |
| | JUMLA | 69 |
| MJINI | DISABILITY SAFARI SHOES MAKER | 12 |
| | TUPENDANE WANAWAKE VIZIWI | 10 |
| | JUMLA | 22 |
| **JUMLA UNGUJA** | **VIKUNDI 23** | **465** |
| | | |
| CHAKE CHAKE | JIIMARISHE GOMBANI | 10 |
| | MATEGEMEO KICHUNGWANI | 14 |
| | JUMLA | 24 |
| MKOANI | NIA NJEMA MTAMBILE | 18 |
| | ZAPDD KENGEJA | 16 |
| | ZAPDD MJIMBINI | 18 |

| | | |
|---|---|---|
| | JUMLA | 52 |
| MICHEWENI | TUPENDANE MAJENZI | 12 |
| | HIRIMU MFASI MAJENZI | 16 |
| | TUJUANE KONDE | 52 |
| | | 80 |
| **JUMLA PEMBA** | **VIKUNDI 8** | **156** |
| JUMLA UNGUJA NA PEMBA | VIKUNDI 31 | 621 |

**KIAMBATANISHO NAMBA 4**

| S/N | CHAMA | MASHINDANO | PAHALA | MWAKA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Shirikisha la mpira wa miguu Zanzibar | Mashindano ya klabu Bingwa Barani Afrika na kombe shirikisho | Zanzibar - Misri | Julai, 2019 | Timu ya KMKM NA MALINDI ziliweza kushirika mashindano hayo ambapo KMKM ilitolewa katika hatua ya kwanza kabisa na timu ya MALINDI ilitolewa hatua ya pili ya michuano hiyo. |
| | | Mashindano ya CECAFA U20 | Uganda | Septemba , 2019 | Timu ya U20 ilifikia hatua ya robo fainali katika mashindano hayo. |
| | | Mashindano ya Senior CECAFA Challenge Cup | Kenya | Novemba, 2019 | Timu ya Zanzibar Heroes ilitolewa katika hatua ya kuingia nusu fainali |
| | | Mashindano ya Wanawake Senior CECAFA Challenge Cup | Zanzibar | Novemba, 2019 | Timu ya Wanawake Zanzibar (Zanzibar Quen) haikufanikiwa kufanya vizuri na kutolewa katika hatua za awali |
| 2. | Chama mchezo wa Taekondo ITF | Mashindano ya Afrika | Uganda | Julai, 2019 | Timu ya Taekowndo ITF wamefanikiwa kupata medali 4 za shaba na 1 ya dhahabu |
| | | Mashindano ya Afrika Mashariki | Darresalaam | Oktoba, 2018 | Timu ya Taekowndo ITF wamefanikiwa kupata medali 4 za gold, 2 za fedha na 2 za bronze |
| 3. | Shirikisho la mchezo wa | Mashindano ya Afrika Mashariki | Kenya | Agosti, 2019 | Timu ya shirikisho la mchezo wa Viziwi haikufanya vizuri katika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Viziwi | | | | mashindano hayo. |
| 4. | Chama cha mpira wa ukuta (squash) | Mashindano ya Afrika Mashariki | Kenya | Novemba, 2019 | Timu ya mpira wa ukuta haikufanikiwa kufanya vizuri katika mashindano hayo. |